ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 29 Novemba, 2016

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, naomba kuweka mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 14

Kuboreshwa kwa Maslahi ya Walimu

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa maslahi ya walimu ni duni, na kwa kuwa wakati wa serikali ya awamu ya tatu iliyoongozwa na marehemu Mzee Idrisa Abdul Wakil, mshahara wa mwalimu ulikuwa ndio mshahara mkubwa miongoni mwa watumishi wa umma nchini. Na kwa kuwa hivi sasa hali hiyo haipo tena.

Je, serikali ina mpango gani wa kuboresha mishahara na stahiki nyengine za walimu wetu nchini, ili kurejesha hali iliyokuwepo wakati huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zote inathamini mchango mkubwa wa walimu katika maendeleo ya taifa. Serikali katika vipindi mbali mbali imeyaangalia maslahi ya walimu. Mbali ya mishahara yao ambayo inalipwa kulingana na sifa zao za masomo na uzoefu wa kazi, walimu wanaofundisha katika skuli mbali mbali na maeneo wanayoishi wanalipwa nauli ya kwenda na kurudi kazini kila mwezi. Hata hivyo, napenda nikiri kuwa kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, mishahara ya walimu kama ilivyo mishahara ya watumishi wengine bado haitoshelezi mahitaji na serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuyafanyia marekebisho mishahara ya watumishi wa sekta ya umma.

Hivi sasa, wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea na hatua ya kuupitia na kuufanyia marekebisho muundo wa utumishi wa walimu ili kuwapatia maslahi mazuri zaidi ikiwa na kuwa na madaraja ya walimu kwa kutegemea kiwango cha elimu na uzoefu wa kazi. Ahsante.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kabla ya kuuliza swali langu Mhe. Spika naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuweza kutekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi, lakini vile vile kuboresha masuala ya afya Zanzibar kwa kujenga hospitali mpya ya Abdalla Mzee ya Mkoani, Pemba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mbali na wizara kuchukua hatua za kupitia na kuyafanyia kazi marekebisho hayo ili walimu kuweza kupata maslahi zaidi.

Je, wizara marekebisho hayo watayafanya lini ili walimu waweze kupata maslahi zaidi ili kuendelea na masuala yetu ya elimu Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama tulivyosema katika majibu yetu ya msingi kwamba hivi sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea kufanyia marekebisho muundo wa utumishi

kwa kushirikiana na wizara inayohusika na masuala haya. Kwa hivyo, wakati wowote mchakato huu utakapomalizika na kupatiwa ruhusa ya serikali na hasa katika kipindi cha bajeti inayokuja suala hili litaweza kutekelezwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwa sehemu ya stahiki za walimu ni pamoja na nauli na posho, sasa naomba kumuuliza swali dogo tu. Katika kumbukumbu zangu wapo walimu wanadai nauli na wapo walimu wanadai posho katika Wizara ya Elimu kwa kazi mbali mbali wanazozifanya ikiwemo kusahihisha mitihani, lakini hizi za nauli ni wale walimu ambao wanasomesha sehemu za mbali, ni nini hatma ya wafanyakazi hawa wanaoidai Wizara ya Elimu katika haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kuna baadhi ya malimbikizo ya maposho lakini pia kuna malimbikizo mengine ya mishahara, na wizara tayari inalifanyia kazi suala hili hatua kwa hatua.

Kwa upande wa posho ya likizo imefikia vizuri na posho nyengine hizi zinazohusiana na nauli na usahihishaji zinafanyiwa kazi, na kwa kweli wakati wowote suala hili la maposho litakuwa limemalizika katika Wizara ya Elimu.

Nam. 94

Tatizo la Upungufu wa Walimu Katika Skuli Mbalimbali

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Tuna tatizo la walimu katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba, na hivi sasa tukiangalia sana kwa ujumla tunaona idadi ya walimu ni wengi lakini ukiangalia skuli za shamba walimu ni kidogo, na wanaotakiwa hivi sasa ni wa sayansi tu.

Je, wizara imejipanga vipi kuajiri walimu wa masomo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa skuli nyingi za vijijini hazina walimu wa kutosha ukilinganisha na skuli ziliopo katika maeneo ya miji hasa kwa skuli za Mkoa wa Mjini/Magharibi. Hata hivyo, skuli za mijini zina idadi kubwa ya wanafunzi ukilinganisha na skuli za vijijini na idadi kubwa ya wanafunzi ukilinganisha na skuli za mijini na idadi ya wanafunzi wa darasa ni kubwa sana, kwa wastani wa wanafunzi wasiopungua 60 kwa darasa moja. Baadhi ya skuli za mjini zina wanafunzi wengi sana katika darasa, kiasi inabidi walimu wawili watumike katika darasa moja, ambapo mwalimu mmoja huwa anafundisha na mwengine huwa anamsaidia. Pindipo kama skuli za mjini zitakuwa na madarasa ya kutosha, wingi wa walimu uliopo hivi sasa utapungua sana.

Kwa upande mwengine skuli za mashamba zina uhaba wa walimu, kutokana na baadhi ya walimu hasa wanawake kuhamia maeneo ya mjini kutokana na ndoa na hulazimika kutumia usafiri wa daladala kufuata skuli wanazofundisha jambo linalosababisha uchelewaji baadhi ya wakati.

Pia, kuna uhaba mkubwa wa walimu kwa skuli za Pemba kutokana na walimu hasa wanawake kutoka Pemba kuomba uhamisho baada ya kuolewa na kutaka kuhamia Unguja mjini, na walimu wengine kupendelea kupangiwa kazi katika skuli za Unguja baada ya kuhitimu masomo yao.

Tatizo jengine ni uhaba wa walimu kwa masomo ambapo kuna uhaba mkubwa wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hesabati ukilinganisha na walimu wa masomo ya Sanaa.

Mhe. Spika, wizara inayafanyia uchambuzi wa kina matatizo yote mawili na itatoa mbinu ya kuyatatua matatizo hayo. Kutokana na ukubwa wa uhaba wa walimu wa Sayansi na Hesabati, wizara itaendelea na hatua ya kuajiri walimu wa masomo ya Sayansi na Hesabati na baadae utafuatia uajiri wa walimu wa masomo ya Kiingereza, Historia na Jiografia. Ahsante.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa ndani ya skuli za jimbo langu la Chambani lina ukosefu mkubwa wa walimu, na kwa sababu kuna walimu ambao wamestaafu 2015, 2015 na sasa hivi tayari wako walimu ambao wameshapewa barua za kustaafu mwaka 2017. Je,

Mhe. Naibu Waziri hatuoni kwamba tunawabebesha mzigo mkubwa hawa walimu waliobakia.

b) Ni lini Mhe. Naibu Waziri utakwenda ndani ya Jimbo langu la Chambani kwa kufuatana na mimi kwenda kuliangalia suala hili la ukosefu wa walimu uliopo hasa ndani ya skuli ya Chambani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli katika Jimbo la Chambani lakini pia na katika majimbo mengine kuna upungufu wa walimu na hasa walimu wa Sayansi. Pia ni kweli katika baadhi ya skuli walimu wamebeba mzigo mkubwa kutokana na sababu mbali mbali lakini ikiwemo kustaafu kwa baadhi ya walimu. Kwa hivyo, wizara katika kuliziba tatizo hili ni kwamba ina utaratibu maalumu wa kuziba nafasi hizi ambazo zimeachwa na wastaafu kila baada ya miezi mitatu tunakusanya takwimu iliyopo baadae tunaomba kibali Utumishi ili kuweza kujaza nafasi yao, nataka ifahamike kwamba zoezi hili tunalifanya kila baada ya miezi mitatu.

Hata hivyo, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za kuajiri walimu wa Sayansi, kwa hivyo jimbo lake nalo pia tutalitizama kwa kuwapatia angalau mwalimu mmoja katika mambo hayo.

Pia swali lake la pili ni suala la matembezi, mimi niko tayari wakati wowote kufuatana na Mhe. Mwakilishi kutembelea jimbo lake. Nasema kufuatana naye, kwa sababu mimi binafsi nimeshakwenda bila ya kufuatana naye, lakini naomba nifuatane naye kwa mara nyengine ili nikaangalie jimbo lake. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuniamsha salama na pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Nashukuru kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri lakini nataka niongezee kwamba sasa hivi serikali imejikita katika masuala ya kubagua wanafunzi kuanzia darasa la tisa kama sikosei kati ya Sayansi na *Art* na takriban ukiangalia masomo yale yanakuwa yote ni yale yale pengine labda ni somo moja au mawili tu ambayo yanabahatika kuwa hayaingiliani katika masomo yale. Na bado nimeona katika mchakato wetu ambao tunaendelea nao sijaona vigezo maalumu ambavyo serikali imejipanga katika kuwabagua wanafunzi wale ili wanapofika madarasa makubwa wawe wanasomea kitu fulani ambacho kimejipanga, wakati miaka ya nyuma ilikuwa mtu anasoma mpaka darasa la kumi na mbili ndio anaweza kuchukua masomo ambayo anayahitaji.

a) Je, serikali haioni kwamba itapoteza baadhi ya vipaji ambavyo wale wanafunzi kwa wakati ambao bado hawajajitambua wanaweza kuwa wamejikita tu katika somo fulani lakini baada ya kuwa katika umri ambao tayari ameshajijua kama mimi natakiwa kulisaidia taifa lakini nafasi hiyo atakuwa ameshaipoteza.

b) Wapo walimu ambao wanataka kujitolea kwa imani zao ili kuendeleza elimu, je, serikali iko tayari kuwapokea ili kupunguza wimbi la ukosefu wa walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sio sahihi sana kusema darasa la tisa ndio wanafunzi wanaanza kuwekwa kwa mujibu wa tahasusi zao, sio sahihi. Lakini utaratibu huu unaanza katika kidato cha tatu, lakini utaratibu huu sio sawa kama anavyosema kwamba labda unaanza kuua vipaji vya wanafunzi, hapana. Vipaji vya wanafunzi vinaanza kujengwa tokea msingi na ndio maana tunapofanya mitihani kwa sasa darasa la sita pale tunaanza kuvibainisha vipaji ambavyo tumevigundua, na vipaji hivi viko vya aina mbili kubwa. Kuna vipaji vya Sayansi tunaanza kuvigundua mapema na tunawapeleka katika sekondari maalumu zilizotayarishwa kwa ajili ya masomo ya Sayansi. Na kuna vipaji vyengine vinagunduliwa katika mambo ya ufundi, tunawapeleka katika michepuo ya namna hiyo, vipaji vyengine vya dini tunawapeleka katika tahasusi hiyo na kadhalika.

Pale inapokuja kidato cha tatu, pale kunakuwa na *general education,* ni masuala ya jumla nayo pia baadaye yanaweza kutenganishwa sanaa na sayansi. Kwa hivyo, fikra ya kwamba tunaua vipaji hii haiko, kwa kweli tunavieleza na tunataka zaidi hivi vipaji tuvigundue mapema, ni muhimu sana kwa kweli na hii ndio hasa Sera ya Elimu ya Zanzibar inavyoelekeza.

Kuhusu suala la pili la kujitolea ni kwamba hivi sasa tunao walimu wengi tu zaidi ya mia tatu na zaidi wanajitolea katika skuli zetu mbali mbali Unguja na Pemba, lakini hatutaki suala hili tulifaradhishe, hatutaki suala hili tulifanye kama ndio lazima au tulifanye ndio kigezo cha kuajiri. Wale wanaojitolea ni kwa hiari yao wapo katika maskuli lakini hatutaki ieleweke kwamba kujitolea kwao ndio sababu ya kupata ajira. Sera ya serikali haiko hivyo, sera ya serikali juu ya suala la ajira inapotokea nafasi tupu inatangazwa anayejitolea asiyejitolea wote wana nafasi ya kuomba. Ahsante sana.

Nam. 53

Tatizo la Maji katika Vijiji vya Nungwi

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Kutokana na umuhimu wa maji katika maisha ya binadamu, na kutokana na usumbufu unaopatikana katika suala hili la maji, hasa katika vijiji vyote vya Jimbo la Nungwi, pamoja na kuwa kunachimbwa visima zaidi ya vitano katika jimbo hilo, lakini bado maji ni kikwazo katika Jimbo la Nungwi na maeneo mengi ya Wilaya ya Kaskazini Unguja.

Je, serikali imejipangaje katika kuirejesha huduma hii ya maji kwa kupitia kisima kikuu cha enzi (Kiashange) kwa kusambaza maji mengi na safi katika maeneo yote ya Wilaya za Kaskazini Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 53 kama ifuatavyo:-

Hapo mwanzoni kisima cha enzi cha Kiashange kilikuwa kinapeleka maji katika maeneo ya Matemwe na Nungwi na maeneo ya karibu yanayozunguka vijiji hivyo, lakini kwa sasa na kutokana na ongezeko la mahitaji kisima hicho kimezidiwa na hakiwezi tena kutosheleza mahitaji ya Wilaya nzima ya Kaskazini 'A' Unguja.

Hivyo, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, kutokana na kufahamu vizuri umuhimu wa maji katika maisha ya binadamu ikaona kuna haja ya kuchimba visima vyengine kwa ajili ya kukiongezea nguvu kisima hicho kupitia Mradi wa *UNDP* na Serikali na kupitia Mradi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (*AfDB*), ili kuongeza uzalishaji na ujazaji wa maji katika matangi ya Matemwe na Nungwi kwa lengo la kuimarisha huduma ya maji katika maeneo yenye ukosefu au upungufu wa huduma katika wilaya hiyo.

Kutokana na jitihada hizo, hali ya upatikanaji maji katika jimbo la Nungwi imeimarika ukilinganisha na hapo awali, lakini bado haijafikia kiwango hasa kinachohitajika kama ilivyotarajiwa kutokana na kukosekana kwa huduma hiyo katika baadhi ya maeneo.

Aidha, serikali kupitia Mradi wa Uchimbaji Visima Zanzibar unaosaidiwa na Mtawala wa Ras-al-Khaimah imechimba tena visima viwili vyengine ambavyo vinahitaji kuendelezwa kwa nguvu za serikali, uongozi na majimbo pamoja na wananchi wenyewe ili kuondosha usumbufu unaojitokeza. Hivyo basi, napenda kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Mwakilishi kuweza kushirikiana nasi kwa hali na mali kuviendeleza visima hivi ili kuweza kuwaondoshea wananchi hao usumbufu wa kupata huduma hii muhimu.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika ahsante, pia ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba niulize swali dogo la nyongeza. Tunajua umuhimu wa kisima cha Kiashange na tunajua umuhimu mkubwa wa visima vyengine ambavyo viko ndani ya Jimbo la Nungwi. Pia tunafahamu kwamba kisima cha Kiashange ndicho kilichokuwa kisima tosha ambacho kinaweza kutosheleza sana wanakijiji wa Nungwi na jimbo zima. Lakini kwa sasa hivi usumbufu bado upo kama kawaida. Je, anaonaje tukakifanya kisima hiki cha Kiashange kikatosheleza kwa kijiji cha Nungwi tu, na hivi vyengine vidogo vidogo ambavyo vipo ndani ya jimbo hilo vikaunganishwa *pump* kwa kusaidia vile vijiji vyengine ambavyo viko ndani ya Jimbo la Nungwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba kisima hiki sasa uwezo wake ni mdogo na ndio maana tukaongezea nguvu, nahisi ingekuwa busara akalilia maji tu na sio lazima yatoke katika kisima fulani. Kwa sababu kutoka katika kisima kile cha Kiashange utapita vijiji vingi mpaka kufikia Nungwi. Nimwambie kwamba, sasa kuna mpango maalumu wa kuongeza kisima cha ziada katika tangi ambalo liko Nungwi Mwanguo badala ya visima viwili kulijaza lile tangi kuna mpango wa kuongeza cha tatu, kusudi huduma hiyo ipatikane vizuri kule. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa maji ni muhimu kwa maisha ya kila siku ya binadamu, lakini baadhi ya maeneo maji yapo mfano kama Ndagoni maji yapo ya kutosha, lakini wananchi wangu wa Ndagoni hupata maji usiku hadi usiku na ukizingatia usiku ni muda wa kupumzika.

Je, ni lini tatizo hili la maji kule Ndagoni litaondoka, na je, kuna tatizo gani linalopelekea hata kama maji yapo lakini wananchi hawayapati ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, tuseme kwamba tumelipokea tutalifuatilia tujue tatizo ni nini na hapo tutasema kuwa lini wananchi wanaweza wakapata maji kwa uhakika.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, ahsante naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa eneo kubwa la Kizimbani na maeneo ya Bumbwisudi kuna visima vya maji ambavyo vimechimbwa na *ZAWA*, lakini sasa hivi maeneo ya Kizimbani, Mbuzini na Bububu upatikanaji wake wa maji ni mgumu sana, inawezekana ndani ya siku tatu maji wakapata siku moja na maji hayo mengi yanapelekwa mjini.

Je, kuna mpango gani wa serikali ambao umeandaliwa na sisi wananchi ambao visima vimechimbwa katika eneo letu nasi tukafaidika na maji hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni bahati njema kwa sababu hivi karibuni nilipanga nifanye ziara kwenye vile visima ambavyo vinaendelea kuchimbwa. Kwa vile sijawahi kwenda na nia hiyo ipo, nitafanya mazungumzo naye kujua siku gani tunakwenda tuone kwa pamoja nini tatizo na namna gani tufanye. Ahsante sana.

Nam. 57

Matumizi ya Fedha za Msaada katika Kuondoa tatizo la Maji

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwanza kwa ruhusa yako kabla sijauliza swali langu nataka lisomeke kama ifuatavyo:-

Hii tarakimu ya Shs. 92 Bilioni sio sahihi, mimi nilipopeleka nilisema 92 milioni *USD*. Baada ya kurekebishwa hapo kwa heshima sasa, naomba kujibiwa swali langu Nam. 57.

Hivi karibuni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ilipokea msaada wa jumla ya Shs. 92 milioni *USD*, kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji hapa Zanzibar, Unguja na Pemba.

Kwa kuwa Zanzibar tuna Majimbo Hamsini na Nne (54). Je, Mhe. Waziri haoni umefika wakati wa kuzitumia fedha hizo kwa kila jimbo Shilingi milioni Moja kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji hapa nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 57 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kutoa ufafanuzi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba, Mradi huu wa *USD* milioni 92 uko katika hatua za awali za maombi yaliyolenga kuimarisha huduma ya maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo chimbuko lake linatokana na ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi huko India, na ripoti ya upembuzi yakinifu iliyofanywa na Kampuni ya *NIRAS* kutoka Denmark mwaka 2012 kupitia *AfDB* juu ya kutatua tatizo la maji mjini. Ripoti hiyo iliainisha maeneo husika.

Hata hivyo, Serikali ya India kupitia mradi huu inatarajia kufanya tena upembuzi yakinifu ili kutoa picha halisi juu ya maeneo na kazi ambazo zitakazofanyika kupitia fedha hizo kwa Mkoa wa Mjini Magharibi. Hivyo fedha hizo hazitoweza kugawika kwa majimbo.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kilio cha Wazanzibari maji hakuna jimbo hata moja katika nchi hii, huna sehemu utakwenda na usikute kilio cha maji, ni kero. Mustakabali wa wananchi wetu wamekata tamaa. Lakini kwa bahati nzuri huko nyuma tumeshuhudia misaada kadhaa katika Mamlaka ya Maji, tumekwenda Welezo pale kulikuwa na mradi tukasherehekea katika ufunguzi lakini majibu mpaka leo hayaonekani, na wale wanaokaa Welezo chini hawapati maji.

Je, kwa kuwa mwelekeo wa fedha hizi zipo na zimeelekezwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, wizara iko tayari kushirikiana na viongozi wa majimbo wenyewe kuhakikisha kwamba kuna visima vilivyokuwa tayari na kuna maeneo yaliyo mazuri kuchimbwa ili maji yapatikane katika maeneo mbali mbali katika Mkoa wetu hasa wilaya ya Magharibi A na Magharibi B ndio kwenye sakata la maji kuliko mengineyo. Wizara iko tayari kushirikiana na Wajumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, wizara iko tayari kushirikiana na viongozi pamoja na wananchi wote kwa kufuata masharti ya mkopo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza kwamba, kwa kuwa *ZAWA* wameshapata miradi mingi sana kupitia *JICA*, *UNDP* na maeneo mbali mbali. Mimi nataka nimuulize hivi katika kipindi cha miaka 15 iliyopita *ZAWA* wamepata miradi mingapi na imetugharimu kiasi gani, na imeweza kusaidia wananchi wa Zanzibar kuweza kusaidia suala la maji kutoweka kwa asilimia ngapi katika majimbo yao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, miaka 15 iliyopita *ZAWA* imepokea miradi karibu minne, ambapo kuna mradi wa *JICA Phase I*, lakini kuna Mradi wa *Techno Co. Corporation* ambayo ilijikita sana *Phase I* na *Phase II* kwenye *capacity building* ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa *ZAWA.* Kulikuwa na mradi wa *JICA* ambao ulikuwa unashughulika sana na mambo ya miundombinu na yenyewe ilikuwa kama *pilot project* katika maeneo ya mjini ambayo ilijikita sana katika eneo la Makadara na sasa hivi inaendelea kwenye sehemu ya Shauri Moyo. Vile vile kuna mradi wa *AfDB* ambao unaendelea na umepokelewa na *ZAWA* ambao umefanywa maeneo mengi, lakini pia na mradi wa Kichina.

Kwa hiyo, miradi hiyo minne imefanyika lakini sasa hivi bado tuna mradi mwengine wa India ambao uko katika maandalizi. Kama alivyosema Naibu Waziri wangu kwamba uko katika upembuzi yakinifu (*feasibility study*).

Vile vile tuna mradi wa Japan ambao sasa hivi pia uko katika maandalizi (*Preparatory Survey*), sasa hivi wanafanya maandalizi ya ukaguzi na mambo mengine ambayo tunatarajia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia.

Kwa hiyo, miradi minne ya awali imeshamaliza muda wake, lakini hii miradi mengine ambayo bado inaendelea na katika hii minne *AfDB* bado haijamaliza muda, lakini bado miwili hii tunaitarajia kuipata. Kwa hiyo, naomba nimjibu hivyo, na ninategemea kwa kushirikiana na wajumbe basi tutaweza kufanya kitu kizuri.

Mhe. Spika, labda niongezee pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Naibu Waziri wangu aliyajibu, lakini mradi wa Milioni 92 US$ wa India tunategemea utasaidia sana na kufikia asilimia kubwa ya kupunguza tatizo ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Ahsante.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana nami napenda kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nampongeza kwa majibu yake mazuri ambayo ametueleza, lakini tumeambiwa kwamba mradi huu umekuja kwa maeneo ya mjini. Je, kwa maeneo ya vijijini ambako kumechimbwa visima vingi, ni lini serikali itafanya mpango wa kuhakikisha kwamba visima vile vinamalizika ili kupatikana huduma hii ya maji safi na salama.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni kwamba serikali inafanya jitihada ya huku na kule kuhakikisha kwamba vile visima vinakamilishwa, kwa kushirikiana na viongozi wa majimbo lakini na namna nyengine. Jitihada hizi yeye inawezekana ikawa ni shahidi, kwamba nimekwenda kwenye jimbo lake kuviona kusudi nipate gharama halisi halafu tukae kitako. Ahsante.

Nam. 136

Kuanzishwa kwa Chombo cha Usuluhishi wa Migogoro ya Wafanyakazi - Pemba

Mhe. Said Omar Said - Aliuliza:-

Itakumbukwa kwamba katika maadhimisho ya Mei Mosi yaliyofanyika Makonyo, Pemba 1/5/2015, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma aliahidi kuanzishwa kwa kitengo cha usuluhishi wa migogoro ya kazi upande wa Pemba katika Bajeti ya 2015/16.

(a) Ni sababu gani iliyopelekea kutotimizwa kwa ahadi hiyo.

(b) Serikali inasemaje juu ya utekelezaji wa ahadi hiyo ili kuwapunguzia usumbufu wafanyakazi waliopo Pemba kufuata huduma hizo Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu anayetupa pumzi zake na tukakutana asubuhi hii hapa tukiwa katika hali ya afya njema.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Said Omar Said wa Jimbo la Wingwi swali lake Namba 136 kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, wizara yangu imeshatekeleza ahadi hiyo kwa vitendo, afisa husika atakayesimamia shughuli za usuluhishi wa migogoro ya kazi kwa upande wa Pemba ameshateuliwa rasmi. Pia afisa huyo amepatiwa mafunzo ya usuluhishi na uamuzi wa migogoro kazini ili aweze kutekeleza shughuli zake hizo kwa ufanisi. Hatua inayofuata hivi sasa ni kumuapisha rasmi afisa huyo kwa mujibu wa sheria.

b) Mhe. Spika, muda si mrefu ujao wafanyakazi wa Pemba nao wataondokana na usumbufu wa kupata huduma hiyo. Wizara yangu imelipa uzito wa pekee suala hilo kwani ni moja kati ya haki za msingi za wafanyakazi. Naomba kueleza kuwa suala hili litamalizika katika kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Spika, ahsante kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Nadhani umefika wakati serikali kuanzisha matawi ya vitengo vyengine vya ajira kama vile Mahakama ya Kazi kule Pemba, ili kuwapunguzia wananchi wa kule gharama kubwa kufuatilia huduma zao huku.

Je, Mhe. Naibu Waziri hili analizungumziaje.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, maelezo yake Mheshimiwa tumeyachukua, na namuahidi kwamba tutayafanyia kazi ili kuona vipi tunalitekeleza suala hili.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Spika ahsante, kwanza nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kututeulia mwanamama katika wizara hii, kesi za wanawake hasa Pemba anazijua moja kwa moja, na migogoro iliyoko Pemba katika wizara hii naamini kwamba anaijua nje ndani.

Mhe. Spika, katika jibu lake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba suala hili liko njiani kuwekwa sawa, lakini namuomba atupe kauli ni lini, kwa sababu kila siku ukienda ni kesho, kesho kutwa, baadae, halafu.

Swali jengine ni kesi ngapi za migogoro ya kazi kwa upande wa Pemba zilizowahi kufikishwa Unguja na kupatiwa ufumbuzi stahiki juu ya masuala yao ambayo wameyaleta.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, suala la migogoro mingapi iliyoletwa Unguja kwa upande wa Pemba na kufanyiwa kazi, Mhe. Spika, naomba nimjibu kwamba suala hili linahitaji takwimu. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa suala hili nitamjibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Swali lake la pili naomba alirejee kidogo.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Spika, swali la pili naomba atoe majibu ya serikali suala hili ni lini litamaliza. Kwa sababu sisi wananchi wa Pemba tukienda katika wizara hii tunaambiwa suala hili litamaliza kesho, keshokutwa, hizi ahadi zimeshakuwa ni za siku nyingi sana bila ya utekelezaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu mama kwamba afisa huyu ataanza kazi wakati wowote baada tu ya kuapishwa. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Mhe. Spika, na mimi nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na pia kwa uteuzi wa Rais.

Mhe. Naibu Waziri kipindi cha nyuma pale Gombani ya Kale kulikuwa na kituo kikiitwa kituo cha Wazee, kile kituo sijui kama kilikuwa *officially* au wazee ambao wanakuwa hawa sehemu ya kuwekwa walikuwa wakiwekwa tu.

(a) Je, nilikuwa nakuuliza kwamba kile kituo kwamba kilikuwa *extension* ya kituo hiki cha Zanzibar cha wale wazee na kama kilikuwa sio *extension* ni lini kitakuwepo kituo cha wazee kule Pemba.

(b) Pemba zamani au hata miaka mingi ilikuwa ni kwamba mara nyengine inatokea kesi nyingi za kutupwa kwa watoto za kuokotwa kwa watoto. Lakini kwa ufahamu wangu ilikuwa watoto wale mara nyingi kulikuwa na watu ambao wasamaria wema walikuwa wakiwachukua na kuwahifadhi au kukaa nao kama watoto wao. Lakini kwa hali inayojionesha uaminifu wa watu katika suala la watoto limeingia katika utata, inawezekana hawa majangili wa watoto wakaanza kutumia mbinu ya kuanza kuwachukua watoto wachanga wale ambao watakuwa na mambo hayo.

Je, ni lini Pemba kitajengwa kituo cha kuhifadhia watoto mayatima na wale waliokosa malezi ya baba na mama.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kituo cha Gombani ya Kale sasa hivi kimehamishiwa Limbani ambacho sasa hivi kuna kituo cha wazee na kiko pale, na hili suala linalochukuliwa na watu wanaona kwamba ni wasamaria wema hasa wanapokuwa watoto wadogo na hatimaye watoto hawa wanapowashinda kwa sababu ya tabia mbaya hutafuta utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanawarejesha katika maeneo yao.

Tuko katika harakati za kuhakikisha kwamba tunatafuta utaratibu utakaokuwa muafaka na unaofaa mapema iwezekanavyo, kuhakikisha kwamba suala hili linachukuliwa hatua. Lakini mpaka sasa hivi taarifa zote zinazokuwa zinapatikana kuhusiana na watoto wanaochukuliwa zinafuatiliwa kwa karibu ili zisipotezwe asili zao wala wasishauriwe vyenginevyo. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 4

Kuimarishwa kwa zao la Karafuu

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza**:-**

Zao la karafuu ni zao ambalo linaingiza mapato mengi sana katika nchi yetu na muitikio wa wananchi katika kuimarisha zao hili ni mkubwa, na hivyo mahitaji ya miche ya mikarafuu yanaongezeka siku hadi siku.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza miche ya mikarafuu ambayo itaenda sambamba na mahitaji ya wakulima kwa mwaka.

(b) Je, ni miche mingapi ya mikarafuu iliyopo kwenye vitalu vyake kwa sasa. Na je, unadhani itakidhi mahitaji ya wakulima waliopo.

(c) Je, Wizara yako imeshafanya utafiti kubaini tatizo hilo na imeshawapatia elimu wakulima ili kuepukana na tatizo la kufa kwa baadhi ya miche baada ya kupandwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye vipengele (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:

Karafuu ni zao muhimu la kiuchumi kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba. Ingawa hapo nyuma kidogo zao hili lilipungua umaarufu wake baada

ya kushuka kwa bei katika soko, na hivyo kuathiri uimarishaji na utunzaji wake.

Matokeo yake ni kuachwa mashamba ya mikarafuu bila ya huduma yoyote, kukatwa miti hiyo kwa ajili ya kuni na majengo, mashamba kupandwa mazao mengine na karafuu kusafirishwa nje ya nchi kwa magendo.

Serikali ilitafakari juu ya tatizo hili na kuunda sera sahihi za kuliimarisha zao hili. Sera hizi ni pamoja na kuimarisha soko la ndani la zao kwa kuongeza bei kwa mkulima.

Aidha, Serikali iliongeza juhudi za kuwahamasisha wakulima kuitunza mikarafuu yao mikongwe na kupanda mipya katika maeneo yaliyo wazi.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo mafupi kuhusu zao la karafuu, sasa naomba nichukue fursa hii kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi masuali yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mwaka huu wa fedha wa 2016/2017 Mradi wa Uendelezaji Mikarafuu umehamishiwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu ambao upo chini ya Shirika la *ZSTC*.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kuona umuhimu wa zao hili kupitia Idara ya Misitu, bado inaendelea na mkakati wake wa kuotesha na kuigawa bure miche 1,000,000 mwaka katika vitalu vyake vya Unguja na Pemba. Sambamba na hilo, Wizara inaendelea na kazi ya kuwashajiisha wakulima binafsi kuotesha miche ya mikarafuu kwa ajili ya matumizi yao wenyewe na ile ya ziada kuwauzia wakulima wenzao wanaohitaji miche hiyo.

Mhe. Spika, Uoteshaji wa miche ya mikarafuu unakwenda sambamba na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kazi hiyo. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti uliojitokeza mwaka huu wa fedha 2016/2017, Wizara inaotesha miche ya mikarafuu kwa kupitia vifungu vyake vya matumizi ya kawaida *OC* ambapo hadi kufikia Oktoba 2016, jumla ya miche 326,063 imeshaoteshwa katika vitalu vya Serikali Pemba ikiwa ni - 229,203 na Unguja - 96,860. Wakulima binafsi nao wameshaotesha jumla ya miche 70,360 ikiwa Unguja 18,280 na Pemba 51,680 na kufanya jumla ya miche yote iliyokwishaoteshwa kuwa ni miche 396,423.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi bado haijafanya utafiti wa kina kuhusu kufa kwa mikarafuu. Hata hivyo tathmini za kuishi kwa

miche iliyopandwa hufanywa baina ya mwezi wa Januari hadi Februari ya kila mwaka na zinaonesha kuwa asilimia 53-54 ya mikarafuu inayopandwa ndio inayomea. Isipokuwa kutokana na ukame mkubwa uliotokea katika mwaka huu inatarajiwa kuwa hali ya kuhuwika kwa miche hiyo inaweza kuwa mbaya zaidi. Miongoni mwa sababu ambazo Wizara imebaini kuwa ni chanzo cha vifo hivyo vya mikarafuu ni kwamba mikarafuu wakati mwengine inapandwa ikiwa bado ni midogo. Tatizo hili huwa linajitokeza sana pale miche mikubwa inapokwisha vitaluni, wakulima wanataka wapewe hata ile miche ambayo bado ni midogo sana. Mche wa mkarafuu ili ustawi vizuri shambani unatakiwa uoteshwe kitaluni kwa miezi 18 au zaidi.

Mhe. Spika, tatizo jengine linalopelekea kufa miche ya mikarafuu ni mabadiliko ya hali ya hewa. Kukatika kwa mvua ghafla, jua kali na kupungua kwa unyevu ardhini nako kwa kiasi kikubwa kunasababisha kufa kwa mikarafuu iliyopandwa. Uharibifu wa makusudi kwa baadhi ya watu kufunga wanyama maeneo yaliyopandwa mikarafuu pia ni sababu nyengine inayopelekea miche iliyopandwa kutohuwika vizuri mashambani.

Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa wakulima wa mikarafuu kupitia mabwana shamba, redio na TV, semina, mikutano na vipeperushi ili kuwashajiisha kutumia mbinu bora za kilimo cha mikarafuu ikiwemo uwekaji wa kivuli wakati wa kiangazi, umwagiliaji maji kwa njia ya matone (*drip irrigation)* na kuendeleza kilimo mchanganyiko ili kuimarisha kivuli kwa mikarafuu michanga. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, kwanza niipongeze Wizara ya Kilimo kwa sera mpya, pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu na ufuatiliaji. Lakini kwa kuwa kizuri hakikosi kasoro, naomba nimuulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa wakulima wengi kila mwaka wanaendelea kuchukua miche ya mikarafuu katika vitalu na kupanda, na kwa kuwa wakulima wengi sasa hivi wamebadilika katika mashamba yao kuyasafisha yakawa safi kama ulivyoeleza hapo, ilikuwa ni tafauti na nyuma.

Je, wizara yako imechukua hatua gani kufanya utafiti ni wakulima wangapi ambao wamechukua miche na kuipanda na ikaweza kudumu na wanaiendeleza vizuri, na baadae kutoa motisha ili iwe ni kivutio kwa wakulima wengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kama nilivyosema tathmini inafanywa kuanzia mwezi wa Januari mpaka

Februari, kwa hiyo kwa mwaka 2015/16 kwa hapa sina takwimu hiyo anayoitaka, kwa kumletea takwimu sasa nitaomba nimjibu kwa maandishi. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, naomba kwanza nimsifu sana kwa bidii yao na jitihada yao wanaifanya kama wizara.

Lakini Mhe. Spika, katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kuna maeneo mawili ambayo kidogo kuna mashamba ya mikarafuu ambayo yanapatikana ni maeneo ya Donge na Mkwajuni Gamba. Pia katika maeneo haya kuna mikarafuu mingi ambayo tayari imeshakufa na wale wakulima sifikirii kwamba kama wana elimu hiyo ya kutafuta miche mingine na kuifanyia kazi kwenye mashamba yao.

Pia katika mashamba yaliopo Donge au wakulima waliopo Donge bado nafikiri hawajauona umuhimu huu wa kurejesha yale mashamba ya mikarafuu na hatimaye mashamba hayo wengine kwa kuuza kuchimbwa mchanga.

Je, wizara inalichukuliaje suala hili na inawapa wito gani wakulima hawa ili kuweza kurejesha mashamba yale kwenye kilimo cha mikarafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza kabisa nikupongeze sana kwa ziara yako uliyoifanya na kutupatia hizi taarifa Mheshimiwa Mwakilishi muhimu sana kwetu sisi Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa tunaahidi kwamba wakulima hao tutawatafuta na tutakaa nao na tutawaelewesha umuhimu wa zao hili la karafuu, vile vile tutawapa miche bure na ikiwezekana *staff* wangu tutawasaidia pia katika kuotesha miche hiyo na kuishughulikia. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Naibu Waziri kuna vitalu vingapi vya wizara na watu binafsi Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema kwamba kuna vitalu jumla ni 396,423 ikiwa binafsi ni miche 7360 na Pemba 229,203 na Unguja 96,860. (*Makofi*)

Nam. 62

Upungufu wa fomu za Kupasishia

Mhe. Shehe Hamad Mattar (Kny Mhe. Mohammed Said Mohammed)– Aliuliza**:-**

Tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kuanzisha Idara ya Usafirishaji. Kuanzia tarehe 1/7/2016 mpaka tarehe 8/7/2016 kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa fomu za kupasishia magari katika Idara hiyo.

a) Ni sababu gani iliyosababisha kutokea kwa upungufu huo.
b) Hatua gani zilizochukuliwa kuzuia upungufu huo usitokee tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 62 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Ni kweli kwamba kuanzia tarehe 1/7/2016 mpaka tarehe 8/7/2016 kulikuwa na upungufu wa fomu za kupasishia vyombo vya moto kulikosababishwa na kukosekana kwa karatasi za kutengenezea vitabu vya fomu hizo katika Kiwanda cha Uchapaji cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

(b) Hatua zilizochukuliwa ni kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuhakikisha kuwa anakuwa na karatasi za kutosha za kuchapisha vitabu vya fomu hizo na nyengine zinazotumiwa na Idara ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, kuwa kuwa wananchi wengi walipata matatizo pamoja na kufikishwa mahakamani na kutozwa faini.

Je, serikali iko tayari kuwafidia wananchi hawa waliopata matatizo kwa wakati huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, katika kipindi chote hichi cha usumbufu sisi tuliwaagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote anayekamatwa na chombo chake kutokana na tatizo lililotokezea na mimi mwenyewe nilifanya bidii za kwenda

mpaka Kiwanda cha Mpiga Chapa ili kuhakikisha kwamba hizi fomu zinatoka na ilikuwa ni kipindi cha sikukuu. Kwa hiyo, kipindi kile chote waendesha gari na pikipiki na vyombo vyengine vya moto waliruhusiwa bila ya kutozwa na kupigwa faini ya aina yoyote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, suala hili la ukosefu wa nyaraka maalumu katika Idara ya Uchapishaji limekuwa likijirejea rejea kwa miaka mingi sana na ukweli linaikosesha Idara yenyewe mapato na serikali kwa jumla. Lakini kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa kipindi cha sikukuu chote hicho mliacha bwerere kwamba ilikuwa kila mtu afanye atakavyo.

Je, wizara yako haioni kwamba wakati umefika wa kukutana na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwapelekea mahitaji ya mwaka mzima kwa makisio yenu ili tatizo hili lisirejee kila mara na kuisababishia serikali hasara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli kabisa suala hili hata mimi liliniumiza kichwa kwani kwa kipindi kile kifupi tulikosa zaidi ya milioni kumi na tano na mimi nilikaa na Mkurugenzi wa Uchapaji na akaniarifu kwamba hili suala hata na wao waliumiza kichwa kutokana na kwamba kulikuwa na urasimu fedha zikitoka wizarani kwetu inabidi tuzipeleke wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha inabidi zipitie tena Wizara ya Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais sasa hizo zote ni taratibu ambazo ziliwekwa. Lakini kama ulivyosema hivi sasa sisi tulivyofanya tumeshapeleka bajeti yetu yote Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba tatizo lile halitokei tena katika Idara ya Usafiri na Leseni. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed:

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameimarisha vya kutosha kiwanda cha Uchapaji cha Zanzibar na kuleta mashine mpya na vile vile kutokana na ubora wa kiwanda chenyewe ni sababu gani zinazosababisha wizara isipeleke kwa wakati karatasi zile.

(b) Kwa kuwa risiti na vitu vyengine kama hivyo Pemba vinakosekana kiasi miezi mitatu, je, huu si uzembe wa wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, nataka kumwambia kwamba wafanyakazi wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kwa hiyo, hakuna uzembe wowote unaotokezea. Kama

nilivyosema mwanzo tatizo hili linatokana na kwamba yale *material* ya kutengenezea zile fomu kwa kipindi kile yalikuwa hayapo katika Idara ya Uchapaji, kwa hiyo wao waliagizia Dar- es Salam.

Mimi pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha alihakikisha kwamba licha ya kwamba tulikuwa katika kipindi cha mapumziko siku za sikukuu lakini watu wale walikwenda kuchukuwa yale *material* na wakaleta na kama nilivyosema mwanzo nina imani kubwa sana tatizo hili hivi sasa halitotokezea tena kwani tumejipanga vizuri na kama litatokeza basi itakuwa katika sehemu nyengine sio kwetu Wizara yetu wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 65

Kufaidika kwa mapato yatokanayo na TCRA

Mhe. Salma Mussa Bilal– Aliuliza**:**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *TCRA* imekua inakusanya mapato mengi sana Tanzania nzima ikiwemo na Zanzibar katika utumiaji wa simu ambazo zimeenea hata vijijini kote hapa Zanzibar.

Je, Serikali ya Zanzibar inafaidika vipi na mapato hayo ambayo hata wananchi wanyonge wa Zanzibar wanayachangia.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba *TCRA* inakusanya mapato ya mawasiliano ya simu kwa Tanzania nzima ikiwemo Zanzibar. Mapato hayo huyawasilisha Hazina Kuu ya Tanzania. Wizara ya Fedha ya Zanzibar huwa inawasiliana na Wizara ya Fedha ya SMT kwa ajili ya kupata mgao wake kama zilivyo sehemu nyengine.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita ni kiasi gani cha fedha kilikusanywa, na Zanzibar ilipata mgao wa kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa swali hili lipo Wizara ya Fedha basi basi mimi nitalichukua na baadae nitamjibu kimaandishi Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri anayehusika. Pamoja na majibu mazuri ya swali la msingi nilikuwa na swali moja dogo sana la nyongeza.

Mhe. Spika, ni vigezo gani ambavyo vinatumika vinavyoifanya Zanzibar kuweza kupata mgawanyo huo wa mapato yatokanayo na mawasiliano ya simu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Vigezo ambavyo vinatumika ni vigezo ambavyo tumekubaliana katika Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Kwa hivyo, vigezo hivi huwa vinaingia katika Mfuko wa Fedha wa Pamoja. Hivyo kama nilivyomjibu Mhe. Salma Mussa Bilal katika swali lake la msingi naye ninamuomba anipe nafasi ili baadae nimjibu kwa maandishi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kumejitokeza tatizo kubwa la matumizi ya simu na kupelekea kudhalilishwa kwa viongozi na wananchi wa kawaida.

Je, ni watu wangapi ambao wamechukuliwa hatua na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Na lini litakomeshwa suala hili kwamba lisiendelee hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Kama tunavyojua ni kweli hivi sasa si katika simu tu bali hata katika mitandao kumejitokeza tatizo hilo. Lakini mimi ninaomba sana wananchi waisome sana

ile Sheria ya Makosa ya Mitandao na vile vile mambo ya simu, kwamba hili ni kosa kubwa sana, na ninamuomba sana Mhe. Mwakilishi awe anatoa elimu kwa watu wake kutokana na suala hili.

Kwa hivyo, masuala haya yote yanapotokezea huwa yanapelekwa Polisi kwa ajili ya mtu mwenyewe yule aliyekosewa kwenda kutoa wenyewe wanasema mashitaka au madai kwa yule aliyemkosea. Katika Polisi kuna Kitengo kinaitwa *Cyber Crime*, na wao kwa kuwasiliana na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali ndiyo zinafunguliwa kesi.

Kwa hivyo kwa hapa Zanzibar mpaka sasa hivi hii Sheria ya Mtandao kama nyote munavyojua ilikuwa haijapitishwa hapa, ililetwa mezani katika Kikao kilichopita. Kwa hivyo mimi nina imani kubwa sana kutokana na Sheria hii basi wananchi watajitokeza kwa wingi wale ambao wanakuwa wanatuhumiwa au kufanyiwa uchochezi wa aina yoyote kupeleka kesi zao sehemu zinazohusika, Polisi.

Nam. 75

Upekuzi wa Abiria Wanaopita Bandarini kutoka Unguja na Pemba

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Aliuliza**:**

Abiria kutoka Unguja au Pemba wanaosafiri kwa njia ya bandari zetu, hupita bandarini hapo bila ya upekuzi wa mizigo yao, na kuhakikisha kuwa ni salama bila ya matatizo.

Kwa kuwa hivi sasa hali ya uaminifu duniani siyo nzuri, je, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha upekuzi wa mizigo na abiria wanaokwenda Pemba au Unguja ili kuhakikisha usalama wa mizigo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba, Wizara yangu imepokea wazo lake la kufanya upekuzi kwa abiria na mizigo wanaosafiri

kupitia Bandari ya Unguja kwenda Pemba na Bandari ya Pemba kwenda Unguja kwa madhumuni ya kuimarisha usalama.

Mhe. Spika, hata hivyo, suala hili litahitaji kuangaliwa kwa kina kupitia Vyombo vya Sheria, Ulinzi na Usalama kwani sote tunajua kwamba Zanzibar ni nchi moja yenye kutumia Sheria moja Unguja na Pemba.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, hali ya usalama duniani haitegemei kuwa ya nchi moja, hata nyumba moja munategemeana na usalama wenu munavyoishi. Kwa kuzingatia wakati tulionao uaminifu wa usalama unakuwa mdogo usioamini mwenzio anayetoka nyumba hii akaingia nyumba hii. Je, kwa kuzingatia hilo ninakubaliana kwamba Mhe. Naibu Waziri anasema Unguja na Pemba ni nchi moja, lakini usalama unategemea kutokana na maisha ya watu wanavyoishi. Haoni ni hatari tuliyokuwa nayo katika nchi moja, yaani kutoka sehemu moja kwenda nyengine panaweza kutokea lolote la kuingizwa bila ya kujulikana wakati hakuna upekuzi wa aina yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Kama nilivyomjibu kwenye swali lake mama Mhe. Ali Suleiman Ali nimemwambia kwamba tunatoa tahadhari kutokana na hayo anayosema, lakini ili kulichukulia hatua ipasavyo sisi tutakaa haraka na vyombo vya Sheria pamoja na vyombo vya Usalama ili kuhakikisha kwamba hili suala tunalifanyia kazi.

Kama nilivyosema mwanzo kabla ya kulifanyia kazi hili suala vile vile itahitajika elimu ili watu wasione nchi moja kunafanyika mambo tofauti, na sisi tunataka kuzidisha utengamano na vile vile usalama wetu wa nchi, na kuonekana kwamba bado Zanzibar ni nchi moja na sote tunakaa kuaminiana.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi ninapenda nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Naibu Waziri sasa hivi kutokana na ukuaji mkubwa wa bandari zetu za Unguja na Pemba, hususan Unguja kuna mizigo inapitishwa ndani ya magari.

a) Ninapenda nijue je, kuna mashine pale ya upekuzi wa mizigo ile ndani ya magari.

b) Kama jibu hapana, Ni namna gani munaweza kujua namna munavyokusanya mapato ya Serikali bila ya kujua mizigo inayopita ndani ya magari yale thamani yake.

c) Basi ata kutafuta...

Mhe. Spika: Mheshimiwa mawili tu

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mawili tu? Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Katika bandari yetu ya hapa Unguja Malindi tuna *scanner* pale ambayo inaona mpaka makontena ndani. Kwa hivyo inajua mzigo wowote uliokuwemo ndani ya ile gari, na hivyo ile gari inakuwa inajulikana kitu kilichomo ndani.

b) Baada ya kuangaliwa na vile vile watu wetu wa Bandari na kupitia na vyombo vya usalama wanatakiwa wazipekue zile gari au mzigo wowote unaoingia pale, hata wenyewe tunasema hata kufungua kontena ili nao waridhike kwamba ile *scanner* ambayo ipo hapa kupitia *TRA*, je, nayo ni kama mashine inayoweza inawezekana ikawa na kosa lakini kwa kupitia binadamu vile vile tunafanya ukaguzi.

Kwa hivyo mizigo yote inayopitia bandarini lazima tuikague na ndiyo maana ukamsikia Mhe. Ali Suleiman Ali akawa ametaka pia abiria wanaotoka Unguja na Pemba tuwapekue. Lakini kwa mizigo yote sisi tunawapekua. Hivyo kutokana na suala hili ninataka kumtoa wasi wasi.

Swali lake la pili kwamba mizigo yote tunaipekua na tunahakikisha kwamba hakuna kitu chochote cha hatari kinachokuwemo katika mzigo ule au mtu yeyote kukwepa kodi kwa kusema kiwango kisichokuwa halisi katika yale magari.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ili kwa usalama wa wananchi wa Zanzibar, wananchi wengi wa Unguja na Pemba wanatumia usafiri wa bandari na hasa wananchi wetu wa Wete wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wanahitaji kuitumia bandari hii ya Wete, na bandari hii sasa hivi inaanza matengenezo na ukizingatia kwamba bandari hii imeanza kufanyiwa matengenezo. Je, ni mkandarasi gani anayeifanyia matengenezo bandari hii.

b) Ili vyombo vyetu vikubwa viweze kufunga gati katika bandari yetu ya Wete. Je, Serikali ina mpango gani wa kusogeza kwenye kina kirefu cha maji kwenye bandari yetu ya Wete ili wananchi waweze kutumia na vyombo vikubwa viweze kufunga gati katika bandari hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Maryam Thani Juma maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ni kweli kabisa bandari yetu ya Wete sasa hivi tunaifanyia ukarabati na kiasi cha shilingi milioni mia mbili zimeshatumika, lakini jina la mkandarasi naomba nichukue baadae nimuarifu rasmi, kwa sababu ni jina gumu kidogo lakini nitamjibu kimaandishi. Lakini ni kweli gati ile tunaifanyia marekebisho kutokana na hali yenyewe iliyokuwepo.

b) Kuhusu kuongeza kina cha maji bado tunaendelea na mazungumzo na wawekezaji tofauti ambao walionesha nia ya kutaka kuwekeza katika kujenga, tunaita gati ile ya Wete kwenye sehemu mbili tofauti. Mpaka sasa hivi mazungumzo yanaendelea, na tuna imani kubwa sana hawa wawekezaji wameonesha nia ya kufanya hiyo kazi. Kwa hivyo pale ambapo itakuwa tayari basi tutahakikisha kwamba na kina cha maji kinaongezwa ili meli nyengine kubwa zaidi ziweze kufunga gati katika bandari ya Wete.

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, kwa kutumia Kanuni ya 37 kwa kuweka *hansard* sawa, naomba muongozo wako.

Wakati Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo akimjibu Mhe. Bihindi swali lake la kutaka kujua ni vitalu vingapi viliopo kwa Unguja na Pemba, alisema kwamba ni laki tatu na sitini na sita elfu, mia nne na ishirini na tatu. Sasa ili kuweka *hansard* sawa. Je, vitalu hivyo ndiyo hesabu hii au hakulielewa swali ambalo aliulizwa.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kwanza hilo swali limeshapita, lakini nitamtaka aliyepewa yale majibu aweze kumuona Waziri ili kuweza kurekebishiwa hayo majibu yake. Tunaendelea Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niendelee tena kumshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake wa hali ya juu hasa katika sekta ya afya ambayo kila kiumbe hai anahitaji sekta ya afya.

Baada ya maelezo hayo naomba wizara au Serikali inipe jawabu muafaka la swali hili.

Nam. 11

Matatizo ya Vipimo vya Tenzi dume

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Wagonjwa wa tenzi dume wamekuwa wakisumbuka muda mrefu kusubiri majibu ya vipimo na kubakia bila matibabu, hata wengine kulazimika kufuata matibabu nje ya nchi.

a) Je, ni sababu gani zinazopelekea wagonjwa kuchukuliwa damu na kwenda kufanyiwa uchunguzi nje ya nchi wakati muelekeo wetu hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa.

b) Je, Kitendo cha wagonjwa kukaa muda mrefu wakisubiri matokeo ya vipimo bila ya kupata tiba tunaokoa maisha yao au tunachangia maisha yao yapotee.

c) Kuna wagonjwa tangu mwaka jana wamechukuliwa vipimo mpaka sasa matokeo hawajayapata, na mmojawapo amelazimika kutibiwa Nairobi na mpaka anarudi Aprili, 2016 matokeo yake bado hayajarudi, nini tatizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, hakuna mgonjwa anayechukuliwa damu kupelekwa nje ya nchi kwa uchunguzi kwa kipimo cha uchunguzi wa damu (*PSA*) kipo Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini pia Hospitali ya Al-Rahma kinapatikana. Inawezekana Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikusudia kuuliza kuhusu vipimo vya nyama kwa ajili ya uchunguzi wa *cancer*.

Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya wakati wagonjwa hutolewa vinyama (*biopsy*) na kupelekwa Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kwa uchunguzi zaidi. Hii inatokana na kuharibika kwa mashine yetu inayoitwa *Microtome*.

Mhe. Spika, kwanza kabisa ninapenda kumpongeza kwa dhati, pia kuupongeza uongozi wa Serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi uongozi ambao hauruhusu kwa njia yoyote ile kupoteza au kutishia maisha ya mwananchi wake. Ushahidi wa hili ni jinsi tunavyoziona juhudi zake katika kuondoa kero mbali mbali za wananchi. (*Makofi*).

b) Mhe. Spika, kitendo cha wagonjwa kukaa kwa muda mrefu kusubiri matokeo ya vipimo, hii ni kutokana na msongamano mkubwa wa wagonjwa uliopo katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili ambao wanasubiri huduma hiyo. Hata hivyo Wizara inajitahidi kufuatilia vipimo hivyo kwa ukaribu zaidi. Kwa kawaida vipimo vinavyopelekwa Muhimbili huwa vinachukua wiki mbili mpaka mwezi mmoja kupata matokeo yake.

Mhe. Spika, Wizara haina taarifa ya vipimo vya mgonjwa aliyetajwa na Mhe. Mwakilishi. Hata hivyo tunaendelea kufuatilia na tunamuomba Mhe. Mwakilishi kutoa mashirikiano kwa Wizara ili kubaini ukweli wa jambo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba na mimi nikubaliane naye Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein

anafanya jitihada kubwa sana, lakini wizara yenu sitaki kutumia lugha ambayo kidogo nzito; wizara yenu jitihada zenu kidogo zipo chini.(*Makofi*)

Mhe. Spika, ushahidi wa hayo mimi nilikuwepo juu hivi sasa, na mara nyingi tukiuliza maswali baadhi ya Mawaziri au Manaibu Mawaziri huwa wasaidizi wao kufuatilia hizi hoja tunazoziuliza humu. Nilikuwepo juu na ninaamini hakuna hata mmoja wa Wizara ya Afya aliyefuatilia kadhia hii.

Mhe. Spika, jitihada anazofanya Rais ni kubwa, na kila mmoja tunaziona hazitaki tochi, utendaji wenu bado ni mzito Mhe. Naibu Waziri, kaa na watendaji wenu mufikie hatua, vyenginevyo vyovyote mutatufikisha pahali si pazuri.

Naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mashine aliyoitaja Mhe. Naibu Waziri *Microtome* lini imeharibika na lini itatengenezwa. Na taarifa nilizonazo mimi nilikuwa na bibi yangu pale mpaka leo keshatangulia mbele ya haki, nilichukua vinyama vyake nikaenda kuvipeleka mimi Dar es Salaam leo mwaka wa nne au wa tatu. Kuna jitihada gani munazozichukua. Hilo la kwanza.

La pili Mhe. Spika, hili kidogo itabidi nizungumze kwa lugha nyepesi. Nitakapokuletea ushahidi wa mgonjwa huyo aliyekwenda Nairobi kwenda kutibiwa na vithibitisho vyake utakuwa tayari kujiuzulu.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri naomba ujibu swali moja tu la mwanzo, hilo la pili achana nalo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ulivyoniongoza.

Mhe. Spika, kipimo hichi lini kiliharibika, naomba aridhie nimjibu kwa maandishi. Lakini ninapenda nimwambie kwamba kipimo hichi sasa hivi tumeshakipata na tumekipata kwa msaada wa ndugu zetu wa Norway na kinafanya kazi. (*Makofi*).

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri unafahamu kwamba *staff* wako wa Chake Chake na Konde wapatao kumi wameambukizwa *TB* wakiwa kazini.

Na swali la pili, je ...

Mhe. Spika: Mhe. Tatu Mohamed Ussi naomba uulize swali moja tu.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Spika, samahani baadae kidogo.

Mhe. Spika: Ni moja tu eeh! Haya naomba umjibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, samahani sana naomba arudie swali sikusikia na akisema naomba anyanyue mdomo.

Mhe. Spika: Mhe. Tatu Mohamed Ussi hebu zungumza kwenye *mic* ili Naibu Waziri akusikie

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Waziri, je, anafahamu wafanyakazi wake wapatao 10 wamepata maambukizo ya *TB* wakiwa kazini.

(b) Je, wizara inachukua hatua gani kuwakinga wafanyakazi hao, ili kuweza kujikinga na maradhi hayo wakiwa kazini. Hilo ndio swali langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimjibu kwa jinsi nilivyomsikia, kwa sababu *mic* inaninyima sauti.

Mhe. Spika, malipo kwa waliopata ajali kazini yana kitengo chake katika Wizara ya Afya na huwa yanalipwa kwa awamu. Kwa hivyo, kama wapo ambao wanalalamika hawajapata malipo yao tangu wapate ajali, basi namuomba Mhe. Mwakilishi ashirikiane na wizara kutubainishia, ili yaweze kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza kuhusu maradhi haya yanawakabili sana wanaume ambao wanazidi umri wa

miaka 40, na matibabu yake yako ya vidonge na ya operesheni. Lakini inasemekana kwamba wale ambao wametibiwa kwa operesheni yako madhara yanawakabili. Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kutueleza ni madhara gani. Pia hali ya Zanzibar kuhusu maradhi haya ya tezi dume ikoje hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nilivyomuelewa ni kwamba anataka madhara ambayo yanasababishwa au madhara ambayo yanatokea baada ya kufanyiwa operesheni.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe naomba ulirudie swali la mwanzo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, Baada ya operesheni yapo madhara inasemekana yanasababishwa. Je, ni kweli kuna madhara baada ya operesheni.

Pili, nilitaka kujua ukubwa wa tatizo hili kwa Zanzibar kwa sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, madhara makubwa ambayo yanatokea baada ya operesheni, ni baadhi ya wagonjwa wetu huwa hawafuati miiko ambayo wanaelezwa na daktari waifuate baada ya operesheni.

Kwa hivyo, wagonjwa hawa ambao hawafuati miiko, basi mara nyingi hupelekea kupata madhara ambayo yanatokana na ukosefu wa kujali au kutumia miiko ile ambayo wameambiwa.

Mhe. Spika: Madhara gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mara nyingi madhara ambayo yanawapata ni kuzuia kwa mkojo, inakuwa ni tabu kupata mkojo na wanapopata wanapata maumivu makubwa. *(Makofi)*

Nam. 32

Kutolewa Kwa Elimu ya Maradhi ya *TB*

Mhe. Ali Khamis Bakari – Aliuliza:-

Ni kwa kiasi gani elimu ya *TB* imetolewa kwa jamii, hasa ukijua kuwa wagonjwa kabla hawajahudhuria hospitali kuweza kujilinda asimuambukize mwenziwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** ugonjwa wa kifua kikuu ni moja kati ya maradhi sugu yanayoendelea kuiathiri sana jamii yetu katika rika zote, hasa kwa wagonjwa walio na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi. Wagonjwa wa maradhi haya hupatiwa matibabu bure kutokana na muongozo na sera za matibabu ya kifua kikuu uliopo.

Mhe. Spika, utoaji wa elimu ya afya juu ya kinga ya kifua kikuu imepewa umuhimu mkubwa ikiwa kama ni kinga ya maradhi haya. Njia mbali mbali hutumika kufikisha elimu hii ikiwemo kupitia vyombo vya habari, vipeperushi, vijarida mbali mbali vya kuelimisha, elimu ya afya inayotolewa katika vituo vya afya na hospitali pamoja na kupitia siku za afya vijijini.

Mhe. Spika, aidha, wizara hivi karibuni imepitia upya miongozo ya kutoa elimu na mabadiliko ya tiba kwa jamii kuhusu kifua kikuu katika jamii pamoja na wafanyakazi wa Afya. Miongozo hii husimamiwa kwa karibu na waratibu wa kifua kikuu na ukoma waliopo katika wilaya zetu. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, vipi kuhusu wagonjwa wa *TB* ambao walishaanza kutumia dawa na baadae wakakatisha. Je, ni mikakati gani ambayo mnaichukua ili kuhakikisha kwamba wanamalizia dozi zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wagonjwa ambao wameshaanza kutumia dawa na kukatisha. Mara nyingi wagonjwa hawa wa *TB* kwanza wanatakiwa wahudhurie *clinic* inayohusiana na magonjwa hayo ya *TB*. Sasa wanapohudhuria elimu pale inatolewa, wanashauriwa na wanatakiwa warudi ili kumaliza. Lakini wale ambao hawahudhurii, kuna kitengo maalumu cha watu wa afya ambao huwa wanapita majumbani kuwafuatilia, wengine huwa wanakimbia na wengine huwa wanapatikana wanashauriwa na kuelezwa na wengine hukubali na kurudi. Kwa sababu wagonjwa wengi tu wenye kifua kikuu mara nyingi huwa ni wale ambao ni *affected* na *HIV*. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, nina maswali yangu mawili ya nyongeza nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri. Je, anajua kama kuna wafanyakazi 10 katika Hospitali ya Chake Chake wameambukizwa maradhi ya kifua kikuu, na wafanyakazi wanne anajua kwamba wameambukizwa maradhi ya kifua kikuu. Kama anajua ni hatua gani Wizara ya Afya imechukua kwa wafanyakazi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakiri kwamba sijui ndio kwanza napata taarifa kutoka kwako, lakini nakuahidi nikiondoka hapa nitafuatilia na pia nijue ni hatua gani ambazo zimechukuliwa, na kama hakuna hatua zilizochukuliwa, basi nitawataka wanaohusika katika wizara waweze kuchukua hatua za kustahili juu yao. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ambaye anajibu majibu mazuri sana.

Mhe. Spika, sasa hivi katika Idara yetu ya Afya huwa tuna kauli mbiu ya kusema tuna maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Maradhi yanayoambukiza alitolea mfano ni kama *TB*, UKIMWI na baadhi ya maradhi mengine. Maradhi yasiyoambukiza ni kama *cancer* kama za matiti, shingo ya uzazi na nyengine chungu nzima. Lakini sasa hivi maradhi haya yanayoitwa yasiyoambukiza ndio maradhi yaliyokuwa mengi na yameongezeka kwa kasi. Sasa swali langu linakuja hapa. Namuuliza Mhe. Naibu Waziri

(a) Je, maradhi haya ni kweli hayaambukizi.
(b) Kama maradhi haya hayaambukizi, inakuaje kuwa yamechukua nafasi kubwa kuliko yanayoambukiza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba maradhi ambayo umeambiwa kuwa hayaambukizi basi hayaambukizi, yakiwemo maradhi ya presha na kisukari.

Wizara inachukua juhudi kubwa kuwaelimisha wananchi kujiepusha na maradhi hayo, kwa sababu hayaambukizi, lakini yakiingia ni shida kukutoka.
Mhe. Spika, maradhi haya yanasababishwa zaidi, kwanza na umri wa mtu. Unapofikia umri fulani basi uko katika hatari ya kupata maradhi ya sukari, presha pamoja na maradhi mengine ambayo hayaambukizi. Kwa hivyo, tunashauriwa sana na naomba nichukue nafasi hii kuwashauri wananchi kwamba wawe ni watu wa kupata mazoezi ya viungo kila siku. Mara nyingi

unapofikia umri wa miaka 35 kwenda juu, basi miundombinu yetu ya kibinadamu mara nyingi inaanza kupungua. Kwa hivyo, katika kipindi hicho binadamu unaweza kupata tatizo lolote. Unaweza kupata *stroke*, presha na mengine. Hivyo, tunashauriwa kitaalamu kwamba tuwe ni watu wa mazoezi. Ukishindwa kufika katika mazoezi, basi hata wewe mwenyewe jiadhibu ndani mwako, unajipa mazoezi yale ambayo unaweza kujipa ili kujiepusha kupata maradhi yasiyoambukiza mapema. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam.149

Umiliki wa Hoteli ya Uwanja wa Amani

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imejenga Hoteli ya Uwanja wa Amani, na kwa kuwa hoteli hiyo imepoteza hadhi yake licha ya kuwa ni hoteli ya zamani.

Je, Hoteli hiyo inamilikiwa na nani hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 149 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, hoteli hiyo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo kwa hivi sasa imekodishwa kwa Mwekezaji wa Kampuni ya *Zege Construction* yenye Makao Makuu yake Dar es Salaam na tawi lake lipo hapa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, je, serikali inapata kodi kiasi gani katika kukodishwa hoteli hiyo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, katika mapato ya serikali kwa mwekezaji huyu, hoteli hii wamechukua wenzetu wa *ZIPA*, lakini pia kwa upande wa wizara kuna mapato ambayo wanapata wizara kwa mwekezaji huyu kwa makubaliano tuliyokubaliana na ni yenye thamani ya dola 5 kwa kila mwezi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini katika majibu yake amesema kwamba hoteli hii imekodishwa kwa Kampuni ya ZEGE.

(a) Je, imekodishwa kwa muda wa miaka mingapi.
(b) Hizo fedha ambazo zinalipwa kwa mwezi ni kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, mwekezaji huyu kwa makubaliano ya pamoja katika mikataba yake, imekodishwa kwa miaka 33.

Vile vile kuhusu malipo ambayo yanapatikana kwa mwekezaji huyu, ni kama nilivyoeleza katika swali la nyongeza lililopita kwamba wizara wanalipwa dola 5 kwa kila mwezi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu ambayo yametolewa na Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, kama alivyoeleza Naibu Waziri kwamba taratibu za kukodishana inakuwa ni taratibu za kiserikali, na mikataba huwa inapitishwa kwa Mwanasheria kikawaida, lakini kwa uwekezaji huu ni uwekezaji uliowekwa kwa miaka 33 kama ilivyo mikataba yetu hukodishwa kwa muda mrefu, miaka 33, 66 au 99.

Kwa hivyo, kwa hoteli iliyokuwepo pale Uwanja wa Amani imekodishwa kwa miaka 33, ambayo itakuwa na *extension* pale, ujenzi pale uwanja wa judo kukamilisha hoteli yenye ghorofa tatu. Hoteli hizo zote zitakuwa ni kwa ajili ya kuwasaidia wachezaji wetu na timu mbali mbali ambazo zinakuja kukaa pale kwa ajili ya michezo.

Mhe. Spika, kuhusu suala zima la fedha ambazo zimekodishwa katika mkataba ule, naomba Waheshimiwa Wawakilishi tuutizame vizuri na tuupitie ule mkataba, kwa sababu hicho kijisehemu kilichotajwa hapo, ni kijisehemu kwa ajili ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, lakini mradi ule ni mradi wa uwekezaji uliopo chini ya *ZIPA*. Kwa hivyo, tutatizama vizuri mkataba tukisha tutamjibu kwa maandishi, ni fedha kiasi gani inayopata wizara yetu kiasi gani, inayopata *ZIPA* kiasi gani na mwekezaji analipa namna gani, tutamjibu swali hili kwa maandishi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Viwe Khamis nilikuona lakini umeridhika. Mhe. Omar Seif Abeid swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nikauliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa katika swali lake la msingi lililoulizwa na muulizaji lilihusiana na hoteli ambazo ni za utalii, na kwa sababu kule Pemba sisi tuna hoteli tatu. Kuna hoteli ya Chake Chake, Wete na Mkoani, ambapo hoteli hizi kama ile ya Wete imekuwa gofu lipo pale halifanyi kazi yoyote.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuziendeleza hoteli hizo ili serikali ikapata mapato kupitia kwenye hoteli hizo.

(b) Ni sababu gani inayofanya hoteli hizo mpaka leo zikaachwa vile vile haziendelezwi. Kama serikali imeshindwa basi ingewapa wawekezaji wakaziendeleza hoteli hizo ili yapatikane mapato. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ukweli ni kwamba pale Chake Chake, Mkoani na Wete kuna hoteli tatu ambazo ni za zamani zinajulikana kama ni hoteli za serikali.

Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi Omar Seif kwamba Hoteli ya Chake Chake imepata ufumbuzi, na Hoteli ya Mkoani nayo imepata ufumbuzi, na kwa sasa soko lililokuwepo hili la afya linatarajiwa hoteli ile kukabidhiwa Wizara ya Afya. Lakini ieleweke wazi kwamba hoteli zile zilikuwa chini ya Shirika la Utalii, jibu hili tulilitoa hapo kabla. Baada ya Shirika la Utalii kuvunjwa basi mali zote zilirudi Wizara ya Fedha ambako kunahusika.

Jibu zuri kwa hoteli zilizobakia kama ile pale ya Wete inaonekana kwamba nayo inahitaji matengenezo, na serikali imo katika hatua za kutafuta njia ya kuiwekeza, na inahisi ikiitengeneza wenyewe halafu ikikodisha ni jambo la aula zaidi, kwa sababu itapata mapato mazuri zaidi kuliko kufanya vyengine. Kwa hivyo, hivi sasa shughuli zote za hoteli zile zinaonekana zinaendelea na muda mfupi ataona zimepata majibu yake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umekwisha, nina matangazo hapa.

Tangazo la mwanzo ni taarifa ya khitma. Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima tunapewa taarifa kuhudhuria kwenye khitma ya wafanyakazi wetu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi waliokwishatangulia mbele ya haki hivi karibuni. Wafanyakazi hao ni kama ifuatavyo.

1. Bw. Khamis Juma Chande aliyewahi kuwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi.
2. Marehemu Biubwa Othman Said; na
3. Marehemu Time Khamis Bakar

Khitma hiyo itasomwa katika msikiti wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, Chukwani kesho Jumatano baada ya sala ya Adhuhuri na tunaombwa tushiriki kwa wingi kuwaombea dua wenzetu.

Taarifa inayofuata ni taarifa ya mechi. Meneja wa Timu ya Baraza la Wawakilishi Sports Club anawatangazia wachezaji wote, wapenzi na mashabiki wote wa timu hii kwamba kutakuwa na mechi ya kirafiki na marafiki zetu kutoka Kigamboni Veteran Sports Club, siku ya Jumamosi tarehe 03/12/2016 mnamo saa moja usiku katika Uwanja wa Amaan, sote tunaalikwa kuhudhuria kwa wingi ili kuwapa moyo wachezaji wetu ikiwa ni kujiandaa na mashindano mbali mbali yanayotukabili hivi karibuni.

Taarifa nyengine ni Mgeni tuliyekuwa naye ni mmoja; mgeni wa Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) huyu ni bwana Wilfred Mushi, ni Mtanzania wa mwanzo kupanda mlima wa *Everest* ni mlima mrefu kuliko yote yaani *point* ya juu kabisa Duniani hiyo, na ni miongoni mwa Watanzania kumi maarufu, ingawa kuna taarifa zaidi kwamba kwa Afrika anakuwa mtu wa tatu kuweza kupanda katika kilele hicho cha *Everest*. Yeye anaishi Moshi na ni mfanyabiashara wa biashara ndogo tu. Ahsanteni *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya shughuli inayoendelea, na baada ya hapo mimi nina shughuli kidogo nje ya hapa, Mhe. Mwenyekiti naomba uje uchukue nafasi tafadhali.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kuendelea na kikao cha Baraza letu tukufu, na kupata fursa ya

kuwasilisha Mswada wa Sheria Mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, itakayochukua nafasi ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 9 ya mwaka 2005.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako na busara na kuwezesha Mswada huu wa Sheria kuweza kuwasilishwa katika kikao hichi.
Mhe. Mwenyekiti, niruhusu kutoa shukurani nyingi sana kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Makamo wake Mhe. Hamida Abdalla Issa na wajumbe wote wa kamati hii kwa kazi kubwa waliyoifanya kuupitia Mswada huu wa Sheria na kupendekeza marekebisho katika vifungu mbali mbali vya Mswada huu.

Pia nawashukuru Makatibu wote wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kuisaidia vyema kamati wakati alipofanya mapitio ya Mswada wa Sheria hii, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imefanya kazi kubwa ya kuandaa Mswada wa Sheria hii, kwa hivyo sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Said Hassan Said na kuwashukuru watendaji wote wa Afisi yake waliohusika na uandaaji wa Mswada wa Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia shukurani za kipekee nazitoa kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar na Naibu Katibu Mkuu ndugu Ali Khamis Juma, kwa kusimamia vyema kazi zote za uandaaji wa Mswada huu tokea hatua za kuifanyia mapitio Sheria ya sasa ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 9 ya mwaka 2005. Juhudi za wote hawa na wengine waliochangia kwa njia moja au nyengine zinathaminiwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, umetayarishwa baada ya matokeo na mapitio yaliyofanywa na Mshauri elekezi kwa masuala ya ununuzi. Matokeo hayo pia yalikuwa na mtazamo sawa na matokeo ya tafiti mbali mbali ikiwemo utafiti wa uwajibikaji katika matumizi ya umma (*Public and Expenditure Financial Accountability)* uliofanyika mwaka 2010 na utafiti uliofanywa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa *DFID* uliofanyika mwaka 2015, utafiti ambao pia uliangalia maeneo hatarishi ya usimamizi wa fedha za umma kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu ukiacha fedha zinazotumika katika ulipaji wa maslahi ya watumishi wa Serikali, eneo la pili linalotumia fedha za umma nyingi ni eneo la ununuzi wa bidhaa na huduma mbali mbali, hivyo endapo eneo hilo litakosa misingi imara ya usimamizi, itaathiri mwenendo

mzima wa usimamizi wa fedha za umma na kuzoretesha juhudi za Serikali na kuwaletea maendeleo wananchi.

Kiujumla kasoro zifuatazo ziliainishwa wakati wa mapitio ya Sheria Nam.9 ya mwaka 2005.

1. Kuwepo kwa urasimu mkubwa katika utekelezaji wa taratibu za ununuzi na uondoshaji wa vifaa vichakavu.

2. Kutokuwepo kwa viwango kwa maana *threshold* kwa kila aina ya ununuzi wa bidhaa, kazi na huduma pamoja na ushauri.

3. Kukosekana kwa muundo wa Bodi ya Zabuni kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa maana ya Mabaraza ya Miji na Halmashauri.

4. Kuwepo kwa tofauti baina ya Sheria na Kanuni juu ya utaratibu wa uundaji wa kamati za tathmini.

5. Sheria imewatambua wakuu wa Idara Maalumu, Mashirika, Idara zinazojitegemea na wakala wa serikali kuwa ni wenyeviti wa bodi za zabuni wakati wao kiutaratibu ni maafisa Wahasibu.

6. Kutowekwa wazi kwa mfumo wa uondoshaji wa vifaa vichakavu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutatua kasoro zilizopo kwa Sheria ya sasa ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma, Serikali imefanya maamuzi ya kuleta mapendekezo ya Kuanzisha Sheria mpya ya ununuzi na uondoaji wa mali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba niwasilishe kwa muhtasari yaliyomo katika Mswada huu ninaowasilisha katika Baraza lako tukufu.

Mswada wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma unaowasilishwa umegawika katika sehemu kuu tisa kama ifuatavyo:

1. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ambayo inajumuisha jina fupi, kutumika kwa Sheria, na Tafsiri ya baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika.

2. Sehemu ya pili inahusu uanzishwaji wa Mamlaka ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, malengo ya mamlaka, kazi za

mamlaka, uwezo wa mamlaka na kuanzishwa kwa Bodi za Wakurugenzi wa Mamlaka, sifa za Mwenyekiti, kazi za Bodi, muundo, muda wa bodi na kukasimu kazi na uwezo.

3. Sehemu ya Tatu inahusu taasisi za ununuzi na uondoshaji wa mali ya umma na inajumuisha uwezo wa taasisi zinazohusika na ununuzi, majukumu ya Afisa muhasibu, bodi za zabuni, kazi za bodi za zabuni, uwezo wa bodi za zabuni, kuanzishwa kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, kazi za kitengo, kazi za idara zinazohusika na ununuzi, kamati ya tathmini, na kukasimu madaraka kwa Afisa Muhasibu kutokubaliana baina ya bodi ya wazabuni na kitengo cha ununuzi, kazi za idara husika, uwezo wa Idara husika, uhuru wa kufanya kazi kuthibitisha kutumia njia mbadala za ununuzi, kumbukumbu za taasisi za ununuzi na uondoshaji wa mali za Serikali, na ununuzi wa uendeshaji katika vyombo vya usalama wa taifa.

4. Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu kanuni za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ambapo inajumuisha utekelezaji wa kazi za msingi, ushindani wa uwazi wa zabuni, uteuzi wa wazabuni bora na upatikanaji wa taarifa za zabuni.

5. Sehemu ya tano Mhe. Mwenyekiti, inahusu mipango ya ununuzi na uondoshaji wa mali, mfumo unaokubalika, mfumo wa uhifadhi, utaratibu mzuri na viwango vilivyokubalika, viwango vya nyaraka za zabuni, uteuzi wa wazabuni, njia za kuwasilisha zabuni, kupokelewa na kufunguliwa zabuni, sifa za msingi za wazabuni, utaratibu wa tathmini, mabadiliko ya taarifa za zabuni, ufafanuzi wa zabuni zilizopokelewa, zuio la kufanya mabadiliko, zabuni iliyokubalika, sababu za kukataliwa zabuni, mikataba na mabadiliko ya mazingira ya zabuni.

6. Sehemu ya Sita inahusu utaratibu wa ununuzi na uondoshaji wa mali ambayo inajumuisha katazo kwa maafisa wa Serikali, kuchagua njia ya ununuzi zabuni za dharura, ushindani wa zabuni za ndani na ushindani wa zabuni za kimataifa. Lakini pia inahusisha uteuzi wa watoa huduma na zabuni ya ushauri ielekee.

7. Sehemu ya saba inahusu aina mbali mbali za mikataba.

8. Sehemu ya Nane inahusu mapitio ya kiutawala, kuvunjwa kwa mikataba.

9. Sehemu ya Tisa ambayo ndio ya mwisho inahusu masharti mengineyo na inahusisha mipaka ya mikataba ya wajumbe wa chombo cha ununuzi na uendeshaji, kinga ya kutoshitakiwa, kanuni za utendaji, kusimamishwa kwa watoa huduma, makosa na adhabu, kanuni, miongozo, mashatri ya mpito, masharti ya kimataifa na kufutwa na kubakizwa.

Mhe. Mwenyekiti Mswada huu una jadweli tano, jadweli hizo ni kama ifuatavyo.

1. Jadweli la kwanza ni kiapo cha tamko kwa Wajumbe wa bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka.

2. Jadweli ya pili inahusu muundo wa bodi ya zabuni

3. Jadweli ya tatu masharti ya kutumia njia mbali mbali za ununuzi.

4. Jadweli ya Nne, Kanuni za maadili ya kiutendaji kazi kwa wafanyakazi wa mamlaka.

5. Jadweli ya Tano utaratibu na ukomo wa viwango vya ununuzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kusema kwamba Mswada wa Sheria unaowasilishwa umelenga kuimarisha eneo la ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa kuweka utaratibu mpya wa kisheria, utakaofuatwa na Taasisi za Umma pamoja na watendaji wakuu wa taasisi.

Matumaini yangu masharti yaliyowekwa kisheria yatafuatwa ipasavyo iwapo sheria hii itapitishwa rasmi na itasaidia kutatua changamoto zilizojitokeza na kuleta ufanisi katika shughuli za usimamizi wa rasilimali za umma na kupelekea maendeleo na ustawi katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny: **Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):** Mhe. Mwenyekiti, Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kutuwezesha kuhudhuria katika Baraza lako tukufu.

Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu mswada wa sheria ya kufuta sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutunga Sheria Inayoanzisha Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti,Kamati yetu inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuamua kuja na Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma kwa lengo la udhibiti bora wa shughuli za ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma. Hii ni kwa sababu, Sheria iliyopo sasa hivi inayo mapungufu ambayo yanahitaji kuboreshwa kulingana na wakati tulionao.

Mhe. Mwenyekiti,Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango wakiwemo Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum na Katibu Mkuu wa Ndugu Khamis Mussa kwa mashirikiano mazuri waliyoyatoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kupitia Mswada huu, hadi leo hii tunausoma katika Baraza lako tukufu, naomba nikiri kuwa kazi ya kupitia Mswada huu haikuwa rahisi kutokana na umuhimu wa Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni muhimu sana katika shughuli zote za matumizi ya fedha za umma, kwani zaidi ya asilimia 70% ya matumizi ya Serikali yanaenda katika manunuzi ambayo hutumia fedha za wananchi.

Mswada huu umekuja kuweka misingi bora ya kuhakikisha kuwa shughuli zote za ununuzi na uondoshaji mali za umma yanafanyika chini ya usimamizi ulio bora. Kamati yangu inaamini kuwa endapo Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataupitisha Mswada huu, manunuzi yote yanayotumia fedha za umma yatakuwa yanasimamiwa katika utaratibu mzuri

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, pamoja na Sheria nzuri tutakazozitunga, lakini kama watakaopewa dhamana ya shughuli hizi hawatakuwa waadilifu bado dhamira iliyokusudiwa na Serikali itakuwa haijafikiwa. Ikumbukwe kuwa katika shughuli za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma mambo manne muhimu yanapaswa kuzingatiwa ili kuleta ufanisi

wa shuguli hizi, mambo yenyewe ni: Uwazi, Uwajibikaji, Ushindani na Kuzingatia thamani halisi ya fedha; mambo haya ndio misingi ya uadilifu katika mchakato mzima wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kutahadharisha sana wakati wa utekelezaji wa Sheria hii juu ya suala la rushwa, yapo malalamiko mengi sana kwa baadhi ya Wazabuni kuhusu suala la rushwa katika masuala ya utoaji wa zabuni. Kamati yangu inamtaka Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ndio msimamizi wa Sheria hii kufuatilia kwa ukaribu sana shughuli zote zinazohusiana na masuala ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, na mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na masuala ya rushwa hatua zinazostahiki zichukuliwe haraka iwezekanavyo ili iwe ni funzo kwa wengine.

Ikumbukwe kuwa, endapo tutaendelea kuwa na muhali katika kusimamia Sheria hii, tutazidi kuitia hasara Serikali, kwani tutakuwa tunanunua bidhaa zisizokuwa na ubora au kupatiwa huduma zisizo na kiwango na hatimaye baada ya muda mfupi kutumia tena fedha nyengine kufanya tena shughuli zile zile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mhe. Waziri pia, Sheria hii inamtaka kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi ripoti ya tathmini ya utendaji kazi ndani ya miezi miwili au katika kikao kinachofuata mara baada ya kupokea ripoti hiyo. Ripoti hii ni muhimu sana kuwasilishwa na inatakiwa iwasilishwe kwa wakati kwa lengo la kuweka uwazi juu ya utekelezaji wa kazi za Mamlaka. Kamati yangu haitasita kumkumbusha Waziri juu ya uwasilishwaji wa Ripoti hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, ni wazi kuwa utekelezaji wa Sheria hii hautakamilika bila ya kutungwa Kanuni zake, kwa hivyo, Mhe. Waziri mara baada ya Baraza lako tukufu kupitisha Sheria hii na kusainiwa na Mhe. Rais, Kanuni za Sheria hii zitungwe haraka iwezekanavyo kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla, Kamati yangu wakati inapitia Mswada huu ilifanya marekebisho makubwa sana katika lugha, kwani kulikuwa na utofauti katika maneno yanayotumika baina ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili, lakini vile vile tulifanya marekebisho ya msingi katika baadhi ya vifungu, marekebisho yote hayo ni kwa ajili ya kuboresha Mswada huu. Kwa ruhusa yako sasa naomba uniruhusu nieleze baadhi ya maeneo ambayo Kamati iliona ni vizuri kuyafanyia marekebisho, lakini vile vile marekebisho mengine yanaonekana katika nakala ya mapendekezo ya marekebisho ya Kamati.

Mhe. Spika, naomba niwambie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa, kwakuwa marekebisho ya Mswada huu yamefuta baadhi ya vifungu jambo ambalo liliepekea kupangua mpangilio mzima wa vifungu vya Mswada huu, na pia limeathiri kuweka rejea za vifungu (*cross references*) katika Mswada; kwa sababu hili ni suala la uandishi (*drafting*) mpangilio wa vifungu na rejea zitawekwa katika hatua za mwisho za kuupanga Mswada.

Katika eneo moja ambalo Kamati yangu ilifanya marekebisho ni kumtoa Afisa Masuuli kuwa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni, hii ni kwa sababu endapo Afisa Masuuli ataendelea kuwa ni Mwenyekiti anaweza kuwa na maslahi sana katika maamuzi ya Bodi. Kwa hivyo, Kamati yangu ilifanya marekebisho katika kifungu cha 29(2), kwa kuweka wazi kuwa Afisa Masuuli hatakuwa mjumbe wa Bodi ya Zabuni.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na baadhi ya marekebisho hayo ya msingi, Kamati pia ilifuta baadhi ya vifungu ambavyo aidha vilikuwa vinajirudia au muktadha uliokusudiwa katika kifungu umeshaelezwa katika Mswada.Vifungu hivyo vilivyofutwa vinaonekana katika marekebisho ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kwa kuzingatia majukumu makubwa aliyonayo Katibu Mtendaji wa Mamlaka, Kamati ilifanya marekebisho kwa kuongeza majukumu ya Katibu Mtendaji wa Mamlaka kama yanavyoonekana katika nakala ya marekebisho ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa uvumilivu wao hadi kufanikisha kuupitia Mswada huu. Sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
5.	Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	Mjumbe
6.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe
7.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
8.	Ndg. Salum Khamis Rashid	Katibu
9.	Ndg. Asma Ali Kassim	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii sasa kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini, utulivu, sikivu na uvumilivu wao

aliouonesha wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii. Nawaomba sana kwa kuwa Mswada huu ni muhimu kwetu na wananchi wetu waujadili kwa kina na hatimae kuupitisha.

Naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye uwezo kwa kutuwezesha kufika hapa leo kwa ajili ya kuzungumza Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali namba 9 ya mwaka 2005 na kutunga sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali na kuweka masharti yanayohusiana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu napenda pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwanzo baada ya Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, kama tumekuwa tuna waheshimiwa tunaiomba sana Serikali ifanye marekebisho ya sheria, sheria zetu nyingi zimepitwa na wakati. Tumeona juzi tulipitisha sheria ambayo Januari mwakani tukiwa hai na uzima, Sheria ya Ushahidi inatimiza miaka 100. Lakini zipo sheria nyingi karibu 300 ambazo zinaonekana utekelezaji wake unaleta vikwazo vingi. Bahati nzuri kwenye kikao hiki huu ni mswada wa pili wa sheria wa Mhe. Waziri wa Fedha na tunatarajia atakuwa nao mswada mwengine wa tatu pengine kesho tukijaaliwa. Sasa kwa nini tusimpongeze kama miswada 3 inafanyiwa marekebisho katika kikao kimoja. Kwa hivyo, ninampongeza yeye lakini pia na watendaji wake chini ya Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa ni kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi pia kuwapongeza sana wajumbe wetu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wetu Mhe. Yussuf Hassan Idd, nao wamefanya kazi na natambua kwamba iliwachukua muda wao mrefu mpaka usiku kuzungumzia marekebisho ya mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, lazima tuishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuangalia hali halisi ya mambo yanavyoenda na kujitahidi kwenda na wakati. Kabla ya kuanza kuchangia lengo langu kwanza niunge mkono mswada huu kwa asilimia 100 na naomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwamba tujitahidi sana tuuchangie mswada huu.

Kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati amesema, suala la manunuzi katika Serikali linatumia asilimia kubwa ya mapato ya Serikali karibu asilimia 70 ya

mapato. Kwa hivyo, tunaona kwamba sheria hii ya manunuzi, moja ya sheria mG44
uhimu sana katika kudhibiti lakini pia katika utoaji wa huduma katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa sababu mambo mengi yanapitia katika daraja hii ama ununuzi ama uuzaji wa Serikali na kwa bahati mbaya sana kutokana na ukubwa wa matumizi yake vinakuwepo viashiria vya ujanja ujanja na viasharia vya kukwepana. Bahati nzuri katika huu mswada badae nitanukuu kuna vifungu vingi ambavyo vikisimamiwa vizuri inawezekana ikaleta tija kwa watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ninashukuru pia Serikali sasa imeamua kuwa na mamlaka ya ununuzi na uuzaji wa mali za Serikali, na mimi naomba mamlaka hii ipewe nguvu, iwe na nguvu. Katika nchi za wenzetu Taasisi ya Manunuzi na Mauzaji ya Vitu vya Serikali inakuwa ndio washauri wa mwisho wa Serikali katika suala hili. Kwa hivyo, na hapa kwetu bahati nzuri katika sheria inasema wataishauri Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi nyengine za Serikali. Tunataka ifanye kazi kwa uwazi, ifanye kazi kwa uharaka na tusiwe na mzunguko mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa 77 wa mswada huu naomba ninukuu majukumu ya mamlaka, kifungu cha 5 hiki cha sheria hii, kinasema:-

a) Kuhakikisha usawa, ushindani, uwazi bila ya ubaguzi na uthamani ya fedha kwa ununuzi na uuzaji na unazingatia viwango vya uhalisia.
b) Kushauri Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika na vyombo vyote vinavyojihusisha na ununuzi na uuzaji kuhusiana na sera, mifumo na uzoefu na pale inapoonekana inafaa kutumika kwa pamoja.
c) Kuweka viwango vya mifumo ya umma juu ya ununuzi na uuzaji Zanzibar.
d) Kusimamia utekelezaji wa masharti na ununuzi na uuzaji wa vyombo husika.
e) Kujenga uwezo na uweledi wa ununuzi na uuzaji wa Zanzibar na kuhifadhi daftari la watoa huduma za ununuzi na uuzaji pamoja na taaluma ya ununuzi.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni majukumu ya mamlaka, sasa mimi ninahisi kwamba ni vyema kwa mamlaka hii kuhakikisha mambo yafuatayo au mimi ninaweza kusema ni mitego ifuatayo:-

1) Mara nyingi wazabuni wanapokuja kuzabuni Zanzibar wakiona pengine kitu cha bilioni nane, yeye anaweza kuweka

bilioni sita na akawa na bei ndogo kuliko wenzake. Lakini baada ya kukabidhiwa rasmi kazi, kwamba kazi sasa umepewa analeta *addendum* yake kwamba sasa kazi hii itakuwa ya bilioni kumi na mbili kutokana nani ambapo wenzake walii-*tender* na hawakupata kwa sababu ilionekana kubwa yeye alitaka sita lakini anakwenda mpaka 12 na tayari wameshafunga mkataba na Serikali, huu ndio ujanja wa kwanza.

2) Kutokumaliza kazi kwa wakati nalo hili ni tatizo ambalo linatukabili katika miradi yetu.

3) Kufanya kazi chini ya viwango. Juzi hapa tulimsikia Mhe. Jaku, akilalamikia kwamba skuli imejengwa inakabidhiwa inavuja. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kwa wale ambao wamefika Micheweni Pemba, Chuo cha Kiislam kinavuja tangu kimekabidhiwa.

Sasa hivi kuna miradi mengine kwa mfano nitoe mradi ambao unajengwa pale Chuo cha Utalii Maruhubi. Mimi ninaamini ule mradi hauwezi kumalizika kwa wakati, kwa mwendo ambao unajengwa wa kusuasua ninahisi kwamba yule mjenzi uwezo hana. Lipo tatizo Mhe. Mwenyekiti, tatizo letu sasa makampuni mengi ambayo yanatujengea hapa hayatoki Zanzibar, ama yanatoka nje ya nchi ama yanatoka upande wa pili wa Jamhuri. Wanakuja kufanya kazi, wanachukua hela wanaenda zao.

Kwanza mimi nishauri Mhe. Waziri, ingawa katika sheria hii hamkuweka kifungu hicho, lakini hata baadae mukiangalie. Tuwe na kiwango maalum cha kazi, kama kazi chini ya bilioni moja mimi ninafikiri Kampuni ambazo ziruhusiwe ku-*tender* lazima ziwe za Zanzibar hapa hapa, kwa sababu nazo pia tutawapa uwezo kampuni zetu ambazo zinalipa kodi ili zisiweze kufa. Sio mpaka kazi ya milioni 500 na kampuni nyengine kutoka nje na wao wana *tender* wanazitaka hizo kazi, kampuni zetu zinakufa na uwezo wa kupata uzoefu unakuwa mdogo. Kwa hivyo, mimi ninashauri kwamba chini ya bilioni moja kazi zingelikuwa zinatolewa kwa Kampuni za Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jengine haya makampuni ambayo yanafanya kazi na Serikali yanachukua fedha nyingi na kwa sababu yanachukua fedha nyingi, mimi ninafikiria pia pamoja na kazi zao hizi nyengine ambazo zimetajwa katika sheria hii, ilikuwa katika sheria itamkwe kwamba lazima wahakikishe kuwa ni walipa kodi wa Serikali ili Serikali fedha zake sio zinachukuliwa, lakini halafu

mtu halipi kodi kama ilivyo kawaida. Lakini pia iwe inahakikishwa kwamba Kampuni hizi ambazo zinapewa *tender* na Serikali zinawalipia wafanyakazi wao katika Mfuko wa *ZSSF* na mambo mengine ya kiserikali.

Kwa ujumla Mhe. Mwenyekiti, mswada huu hauko vibaya sana, isipokuwa uboreshwe zaidi kuhakikisha kwamba hii sheria ikipita inafanyiwa kazi. Ninashukuru kwamba kifungu namba 15(3), ipo fursa kwa yule ambaye alipewa kazi na kunyang'anywa pengine kukata rufaa. Kukata rufaa ni jambo zuri katika demokrasia hata ya utendaji kazi, katika manunuzi na demokrasia nyengine wanapewa fursa wakate rufaa.

Lakini Mhe. Waziri, zamani tulikuwa tuna mazoea ingawa siku hizi naona yanapunguzwa punguzwa sana pengine kwa mabadiliko ya dunia. Lakini katika wale wajumbe ambao Mhe. Waziri, anapewa fursa, kuna wengine wanaingia kutokana na nyadhifa zao za kiserikali, lakini wapo wajumbe kama watatu wanaingia kutokana na maoni au ushauri na baadae Mhe. Waziri, kuona Wazanzibari wote ambao wanafaa. Zamani bodi nyingi ingawa kwa Bara naona wanaliondoa ondoa na hapa msimamo sijaujua wa Serikali walikuwa wanaingia Waheshimiwa katika bodi mmoja ili kuhakikisha kwamba pengine maslahi wa wananchi na wao wanakwenda kuyatetea na zaidi katika bodi kama hizi muhimu.

Sasa kama hilo halikatazwi basi pengine Serikali ingelikuwa inafikiria sana kufanya hivyo ili na wao kuhakikisha kwamba katika bodi nyeti kama hizi wanasaidia kutoa maoni yao na kuisababishia Serikali iende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi sikuwa na mengi isipokuwa niseme tena naunga mkono mswada huu na nawaomba Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi wachangie mswada. Mswada huu ni wa manunuzi ambao unatumia fedha nyingi za Serikali.

Lakini la mwisho kabisa nilikuwa nimelisahau kwamba tunatumia bodi za wanunuzi wakati mwengine tunapata bidhaa ghali zaidi kuliko katika bei la soko la kawaida. Sasa na hili sijui Mhe. Waziri, ameliangalia vipi, kwa sababu unaweza kukuta kwa kupiia *tender board* au zabuni unaweza kukuta chupa ya maji inauzwa shilinge elfu tatu. Lakini chupa ya maji ile ile katika soko la kawaida bei yake ni 500 au 1000, hili ni mfano tu au unaweza ukakuta gari wako katika *channel* ya kawaida gari ile pengine milioni 50. Lakini kwa kupitia *tender board* zabuni unaikuta gari milioni mia moja au mia moja na hamsini, hili nalo Serikali iliangalie italifanya vipi kwa sababu nalo linazidisha matumizi zaidi katika suala la Serikali na pia matengenezo ya magari na vifaa vya

Serikali nalo hili ni tatizo na linaleta changamoto kubwa katika matumizi ya serikali.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hapo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii pamoja na kwamba dokezo langu ambalo liko kwako nilikuwa naendelea kuchangia kwa maandishi, lakini kwa sababu umenipa fursa hii ninafikiri yale ambayo nilitarajia niyawasilishe kwa maandishi basi nichukuwe fursa hii kuweza na mimi kutoa mchango wangu katika mswada huu ulio mbele yetu unaohusiana na masuala ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya michango yangu michache mno kwa sababu si mtaalam sana wa mambo haya ya ununuzi, nitoe tu shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kuweza kwa umahiri wake kuwasilisha hotuba yake juu ya mswada huu muhimu sana kwa wakati huu kuhusiana na suala la ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma.

Lakini vile vile nichukuwe fursa hii kuishukuru Kamati inayohusiana na fedha kwa uwasilishaji wao wa ripoti yao na marekebisho yao mengi ambayo kwa ufupi yametunyima au yametupunguzia ile michango ambayo tulikuwa tunaitarajia. Nishukuru sana na nimpongeza sana Mhe. Gerei kwa uwasilishaji wake mzuri.

Pia, nimshukuru mjumbe mwenzangu Mhe. Machano, ambaye ametangulia kufungua dimba katika uchangiaji wa mswada huu uhusianao na ununuzi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze sana kwa walioona kuna haja ya kufanya marekebisho ya jina la mswada huu katika ukurasa wa 68. Katika uchambuzi wangu katika mswada wa awali ambao tuliupokea na mimi nilihisi kulihitaji marekebisho katika jina la mswada huu ingawa mimi nilikuwa tofauti kidogo.

Mimi nilikuwa pendekezo langu jina la mswada huu lisomeke kwamba; “Mswada wa Ununuzi na Uuzaji” kutokana na lile neno la mwanzo ambalo ilikuwa ni manunuzi na uuzaji. Lakini wenzangu wameenda mbali zaidi wakaona neno 'ununuzi' liwepo, nashukuru na naungana nao kwa sababu katika mustakabala mzima wa lugha ya Kiswahili kwenye upatanishi wa sarufi hakuna neno 'manunuzi', isipokuwa najua tu kwamba pengine tumelirithi kwa wenzetu wa Bara ambao walianza na sheria hii. Lakini niungane nao kwa kuweza kuliona kwamba neno “ununuzi” liondoke kuwe na 'uondoshwaji wa mali za umma' kutokana na mapana yake kwa neno lile la Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hiyo mswada huu nilipoupitia pamoja na kurekebisha jina, lakini humu ndani bado neno 'manunuzi' limejitokeza mara nyingi sana. Kwa hiyo, niombe sana kwamba neno hilo kila lilipojitokeza ili liendane na mnasaba wa jina basi neno 'manunuzi' liwe linaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nije kidogo katika ukurasa wa 72 kwenye tafsiri ya neno 'kosa la rushwa' imesomeka hapa kwamba, inajumuisha 'kutoa, kupewa, kupokea, kushawishi kitu cha thamani ambacho kitapelekea mtumishi wa umma katika manunuzi'. Mimi hili neno 'katika' ukiacha hii manunuzi ambayo tayari nishasema niliona kwamba kama pawe na neno 'kufanya ununuzi', itapelekea mtumishi wa umma kufanya ununuzi na sio katika manunuzi.

Lakini ukija katika ukurasa wa 73, sina hakika kama kamati iliwahi kuliona kwa sababu marekebisho yake ukweli ni mengi sana, lakini kuna neno 'mzabuni'. Hili neno 'mzabuni' limejitokeza mara mbili katika mswada huu, kwa hiyo, niombe kwamba hilo neno libaki moja badala ya mawili. Na katika ukurasa wa 75 penye neno “ununuzi” ilikuwa kunahitajika kineno kidogo hapo kiunganishe katika “yake na upatikanaji” na badala yake isomeke “maana yake ni upatikanaji” halafu itaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 78 katika kifungu cha (e), neno “ruhusa” limegandana na neno “ya” sijui kama wenzangu waliliona lakini panahitaji kuwa na *space* ili kuona kwamba maneno hayo mawili yanasomeka vyema. Lakini kifungu cha (g), pana neno 'kuthibiti' nafikiri kama nimesoma vizuri ilitakiwa iwe neno 'kudhibiti', kwa hiyo, baada ya kutumia “th” basi ije “dh”.

Kifungu cha (i); 'kinasomeka kufanya ukaguzi wa muda wa nyaraka na mwenendo wa uendeshaji wa vyombo vinavyojihusisha na uuzaji na ununuzi'. Inasomeka vizuri lakini kutokana na maudhui na mantiki ya mswada huu umeanza na ununuzi, sijui kama hii uuzaji itakuja ondoka liingie lile la uondoshaji wa mali lakini hapa ililazimika ianze na neno “ununuzi” halafu lije “uuzaji” au lile ambalo limependekezwa libebe nembo ya jina la mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni makosa madogo madogo ambayo niliyaona baada ya kupitia mswada huu. Lakini nikija katika suala zima la ushauri. Mhe. Mwenyekiti, suala la ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma lina matatizo mbali mbali katika taasisi zetu za serikali. Bahati nzuri mimi ni mmoja kati ya wajumbe wa kamati na tumetembelea katika taasisi mbali mbali, tumeweza kuona matatizo mbali mbali ambayo kamati pia itaweza kuja kuleta ripoti yake hapo baadae. Lakini jambo moja ambalo linajitokeza ni suala la mali zinazonunuliwa au majengo yanayojengwa ambayo hayaendani na thamani

halisi ya pesa ambazo zimetengwa. Hili limekuwa ni tatizo katika wizara mbali mbali na mwenzangu Mhe. Machano, aliwahi kuligusia, lakini sisi ambao tunapita katika mashirika na mawizara tumeshuhudia matatizo mbali mbali kuona suala la ununuzi lina matatizo katika vitu vinavyonunuliwa au majengo yanayojengwa kuona kwamba hayaendani na thamani halisi ya fedha ambazo zimetengwa.

Kwa hiyo, niombe sana inawezekana sheria iko vizuri lakini tunazungumza kila siku juu ya utekelezaji wa sheria. Kwa hiyo, hili tulione wizara inayohusika ilione ili kuona kwamba fedha za wavuja jasho wa nchi hii zinatumika vizuri katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu, vyenginevyo, utakuta kwamba serikali inaingia hasara kutokana na uadilifu mdogo wa watumishi wachache wanaohusiana na fani hii ya ununuzi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo kwa kweli linaniumiza kichwa sana na wenzangu, ni suala zima la huu uondoshwaji wa mali za umma. Unaweza ukakuta kuna chombo kama gari pengine imenunuliwa kwa fedha nyingi ambayo pengine hailingani fedha ile ina thamani lakini ukiacha hilo ile *disposal* yake utakuta kwamba inachukua muda mfupi.Unaweza ukaikuta gari imenunuliwa lakini baada ya miaka minne utakuta kwamba imefanyiwa *disposal* ambayo kwa pesa kidogo wakati gari ile ilinunuliwa kwa pesa nyingi sana.

Kwa hiyo, hii ni hatari ndio utakuta lazima sheria zetu ziweze kuangalia vizuri zile mali ambazo zinahitaji kuondolewa zitazamwe hali yake vizuri ili kuona kuna haja ya kuziondoa zisiendelee kutia hasara serikali, lakini vile vile kuepuka ujanja ujanja ambao unafanywa ili kuona mali zile zinaondolewa na pengine thamani yake inayopewa ni ndogo mno. Hili litarejesha nyuma sana yale tunayoyatarajia, kwa hiyo, kuna haja ya taasisi inayohusika yakuweza kufanya tathmini nzuri ya mali za serikali na kuweza kuona kwamba kama zinahitaji kuuzwa basi iwe zinauzwa kutokana na uhalali wake.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona vile vile katika bodi hizi ambazo zinahusika na upitishaji wa tenda mbali mbali. Nina imani kwamba sheria hii itaweka vizuri zaidi kwa sababu kulikuwa kuna kasoro ya sheria iliyopita kuwa bodi hizi sasa zitakuwa makini lakini pia zitakuwa na utaratibu mzuri. Tatizo ambalo linajitokeza katika taasisi mbali mbali za serikali na mashirika ya umma utakuta baadhi ya ununuzi wa vitu na uondoshwaji wa mali unafanywa bila ya kuwekwa vikao vya bodi inayohusika. Utakuta watu wachache tu au inawezekana wakati mwengine mtu mmoja tu anaweza kutoa maamuzi yakuweza kufanya mali iuzwe au ununuzi ufanyike wakati kiwango cha fedha

ambacho kilitakiwa kitumike kinaendana na ile sheria, lakini yeye katumia uwezo wake kuweza kufanya ununuzi bila kuishirikisha bodi. Hii inasababisha kwanza kutoshirikishwa kwa wajumbe lakini vile vile inachangia kuleta minong'ono au manung'uniko katika taasisi mbali mbali kutokana na viongozi wachache kufanya maamuzi ya ununuzi kinyume na utaratibu wa kwenda katika bodi inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri, awe mkali sana katika masuala haya ya ununuzi na kuona kwamba bodi zinazohusika ndizo ambazo zitakuwa zinakaa na kuweza kupitisha maamuzi ya ununuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kingine ambacho kinafanyika bodi nafikiri zinashindwa kuweza kuwaalika na nafikiri kama sheria haipo hii lakini ni muhimu iwepo. Kuna baadhi ya bidhaa, kuna baadhi ya kazi zinahitaji *classification* ya kuweza kuona kwamba kitu kinachotakiwa au mradi unaotakiwa kujengwa basi unakuwa na vigezo ambavyo vinaendana na nchi yetu. Sasa bodi inaweza ikafanya maamuzi bila ya kuwa na mtaalamu ambaye angeweza kutoa *justification* ya kile ambacho kinatakiwa kujengwa au kinachotakiwa kununuliwa. Kwa mfano, inaweza ikawa wizara ina haja ya kununua gari mathalan, lakini gari pengine ambayo imepitishwa kununuliwa pengine *spare parts* zake kwanza ni ghali au inawezekana hazipatikani vizuri katika nchi yetu. Lakini pengine ikapitishwa kununua aina ya gari ile matokezeo yake ni kuja kuona kwamba gari ile pengine inachukua muda mfupi kutokana na kwamba inapoharibika kutengenezeka kwake kunakuwa kugumu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata ukienda katika *contract* za barabara bado hatujawa na vigezo vya kitaifa barabara gani hasa za kiwango gani hasa, zenye sifa gani tunazozitaka. Kwa hiyo, inaweza ikapitishwa hiyo kwamba tunataka barabara tu lakini ikishakujengwa ndio ambayo tunaweza tukaja tukawa tunajilaumu kwamba barabara ile imechukua muda mfupi, ina nyufa, ina mashimo, lakini kumbe *contractor* hakupewa vigezo hasa vya barabara gani tunaitaka katika eneo hili. Nafikiri wakati sasa umefika wa kuweza kufikiria vigezo mbali mbali vya kazi, vya bidhaa na majengo ambayo tunayataka ili mkandarasi anapopewa hiyo kazi basi aone kwamba anaweka vile vigezo ambavyo sisi tumemuwekea, vyenginevyo, tutajengewa barabara ambazo ziko chini ya kiwango, tutajengewa majengo ambayo yako chini ya kiwango kwa sababu tumeshindwa kuweza kuweka vigezo hasa tunavyovitaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sikujiandaa kuzungumza mengi kwa sababu nilikuwa katika mchango wa maandishi na mimi niseme tu kwamba nauunga mkono Mswada huu wa ununuzi kwa asilimia 100 ili tuweze kuona sasa

tunakuwa na sheria madhubutu ambayo itaifanya nchi yetu kuweza kutumia pesa yake vizuri na kwa thamani ile ambayo inatakiwa ili tuweze kupiga hatua kubwa ya maendeleo katika miaka ijayo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji wa mada hii ya leo inayohusu Sheria ya Manunuzi na Uuzaji ambayo itawezesha kuundwa kwa mamlaka ya kazi hiyo.

Kwanza kabisa mimi napenda niipongeze sana Wizara ya Fedha kwa kipindi cha muda mfupi sana karibu mwaka imeweza kuonesha kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa sana na mazuri huko mbele tunakokwenda.

Pili, niipongeze kwa kuundwa hii mamlaka, nadhani matumizi yatakwenda vizuri na kwa vile inavyotakiwa, maana matumizi yakienda kiholela au yakienda kwa matakwa ya mtu kwa malengo ama ya kujinufaisha mwenyewe au vyovyote vile manunuzi hayo yanaisababishia serikali hasara na hata ukiwa mtu binafsi pia kama atafanya matumizi ambayo yatakuwa kiholela basi atakula hasara, atakuwa anawanufaisha wale wengine na yeye anakula hasara.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya manunuzi au utaratibu wa manunuzi na uuzaji unaenda sambamba na mambo ya tenda na unabebwa vizuri sana na mambo ya taratibu nzuri za kuweka *asset register* na kadhalika na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona kama walivyosema wenzangu kwamba tumepita katika mawizara mbali mbali tumeona kwa kweli manunuzi na uuzaji hauendi kwa vile ambavyo inatakiwa kwa lengo la kufanikisha maendeleo. Utakuta manunuzi yanakuwa ama ni makubwa zaidi kuliko vile ambavyo soko lipo na hii inatokana na sababu kwamba ule utaratibu mzima bado haujafatwa kikamilifu. Nasema wakati tunanunua kuna utaratibu huu wa tenda na hii tenda inafanywa na *tender board*. Sasa kama tenda inafanya na *tender board* wale wajumbe wa *tender board* wanapaswa wawe na sifa zile zinazotakiwa kwa tenda ile ambayo inakusudiwa. Na hizi tenda zinakuwa ama tenda za ndani au tenda za nje, zote hizi zinahitaji kukaliwa na *tender board* chini ya uenyekiti na ukatibu wa *procurement officer* pengine au yeyote yule aliyekusudiwa na wajumbe ambao wanastahiki ili manunuzi haya yafanyike vizuri. Kwa hiyo, nasema hii sheria imeweka wazi mambo yote hayo, lakini sisi hapa tunaposimama huwa tunatoa mchango kusisitiza mambo yale muhimu au ile mikakati muhimu iweze kufatwa ili upotevu wa fedha kiholela usiwepo.

Kwa hiyo, napendekeza sana hii mamlaka isimamie *tender board* zote za wizara za serikali na mashirika ili mfumo wa *tender* uwe wa aina moja na uende kwa faida kama ambavyo tunakusudia uende.

Hapo hapo kwenye *tender board* ni kwamba *tender board* hizi zisisitize kufuata ule utaratibu wa kukaa kila panapohitajika ili ununuzi huo ufanywe kiadilifu zaidi. Sasa *tender board* kwa sababu inakaa na kununua basi hata ile *delivery system* nayo iwe *monitored,* iangaliwe ili huko inakokwenda kuwekwa kwenye *store* nako kuwe na *store ledger* ili bidhaa ile iwekwe au pamoja na kuwekwa basi iwekwe kwa utaratibu ambao itadumu.

Halafu mwenzangu alizungumzia pia mambo ya *asset*, tunakuwa na *asset* nyingi; kama *asset* za magari, *asset* za nyumba na kadhalika. Sasa ukiangalia zile *methods* za *depreciation* zinazofanywa utashangaa, inafanywa pengine *linear method of depreciation* ambayo kwa kweli kila mwaka inapungua, utakuta kitu kinapungua kinafika thamani ya *zero* bado kizima. Sasa kama hakuna *re-evaluation* ndio yanatokezea matatizo kama hayo aliyosema Mhe. Mjumbe aliyepita, kuuzwa kitu cha bei ya thamani kubwa kwa bei ya chini kwa sababu hakuna *re-evaluation*.

Halafu na hii *system* ya *linear depreciation* nayo inaweza kuwa na matatizo, kwa sababu kila siku thamani hiyo hiyo, *percentage* hiyo hiyo, inakwenda mpaka tena inakuwa *zero* kama nilivyosema ni matatizo. Sasa hii mamlaka isimamie ili kuwe na utaratibu maalum wa kufanya *re-evaluation* kila mwaka au kila baada ya miaka miwili au mitatu ili thamani ya kile chombo kiwe kinakuwa *monitored,* yaani kinaendelea. Utaratibu huu pia utasaidia hata matunzo kwa kufanyia *maintenance* kama ni magari, majumba ili yale maisha yake yawe makubwa zaidi, kwa sababu nyumba au gari bila ya *maintenance* pia inaweza kuchakaa kwa miaka miwili au mwezi mmoja ikawa haiwezi kwenda tena.

Kwa hiyo, naishauri sana hii mamlaka inayoundwa ya kusimamia mambo hayo ya *procurement* kwa vile ambavyo yataleta faida kuwba kwa serikali.

Pia, katika ziara zetu huko tumeona kwamba pamoja na kuwa *asset register* ama hatuna au zipo bado kwa mule ambamo simo mfumo wa *asset registration* hauridhishi. Kwa maana itaikuta karatasi tu imeandikwa kuna kitu hiki, hiki na hiki; pengine kimeandikwa pale lakini hakipo kiko sehemu nyengine. Sasa hata ukitaka kukifanyia kazi huwezi kukipata. Kwa hivyo, nasisitiza kwamba masuala ya *asset registration* na masuala ya *tendering system* haya yafanyike kwa uangalifu ili bidhaa zisipotee ovyo. Hata kusimamia kwenye mawizara na

kwenye sehemu zote za mashirika kuona kwamba kila *item* ya serikali inafanyiwa *coding* inaandikwa *code* ili ijulikane kwamba hii ni mali ya serikali ili ukitaka kufanya *audit* unakuta kitu kile kinaonekana kipo moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mchangiaji aliyepita kachangia vizuri sana na kachangia michango mingi, nikiendelea kuchangia sana mimi nitakuwa narudia yale yale ambayo kwa kweli yameshasemwa na mengine yameandikwa hapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe niseme kwamba baada ya kusema haya naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naiombea sana hii bodi, hii mamlaka itakayoundwa ifanye kazi zake vizuri sana ili huu upotevu uliokuwa ukifanyika wakati wa kununua na kuuza bidhaa za serikali uondoke, iwe tena hakuna upotevu wa namna hiyo serikali isipate tena hasara.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mhe. Ali SuleimanAli (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili tukufu na hasa tukizingatia kwamba wajibu wetu kupitia miswada mbali mbali na kuielekeza serikali kwa hatma ya faida ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu niseme tu kwamba naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuona pana haja ya kuhakikisha kwamba utaratibu mzima wa sheria zetu za ununuzi na uondoshaji unawekwa vizuri kwa faida ya serikali. Lakini nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake, nampongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na wajumbe wake kwa kufanya marekebisho makubwa na kuweka sawa mswada huu ili ueleweke kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, azma ya serikali ni sahihi kwa sababu tumeshuhudia mengi huko nyuma tunakotoka, utaratibu wa ununuzi na uendeshaji ulikuwa unakwenda kivyake vyake, ndio maana serikali ikakaa na kufikiria kwamba hivi sasa kila litalofanywa liwe katika mwelekeo wa kuhakikisha kwamba uwezo wake au faida inaingia katika pato la serikali na serikali iweze kufanya mambo yake kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kuona mambo mengi ya serikali, tuje katika mali chakavu huwa zinakwenda katika utaratibu ambao wakati mwengine hauelekei. Kwa mfano, mimi niko wizara au shirika au kampuni fulani nafanya kazi kwa utaratibu ambao umepangwa kisheria, lakini kuna kitu nakitaka pale

basi naweza kufanya mipango yangu kiajabu ajabu kitu kile nikakinunua. Kwa mfano, gari au kitu chengine kwa njia ya urahisi ambapo kama utaambiwa na una uchungu wa nchi yako basi machozi yanaweza kukutoka. Serikali ndio maana ikakaa na kufikiria kwamba ni vyema tukaelekea katika mwelekeo wa kutunga sheria nzuri na kuhifadhi haya mambo yetu kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mpango huu sio mbaya kwani tunazingatia kuwa lolote litalowekewa utaratibu uwe na msimamizi anayekubalika kisheria, ndio maana kuna bodi za wazabuni. Lakini kwanza hii bodi ya wazabuni tegemeo langu mimi na ndivyo ilivyo naishauri sana wizara wawe watu waaminifu na waadilifu sana katika serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunashuhudia baadhi ya maeneo yanakwenda mambo wakati mwengine kienyeji akija Shihata apewe, ile itakuwa haileti faida katika ununuzi na uondoshaji katika sehemu zetu hizi ambazo tunaweka kwa ajili ya faida ya serikali. Serikali ina mpango wake wa matumizi, kitu fulani kitatumika baada ya kuchoka au kuonekana hakifai ni vyema kikaondoshwa, lakini katika kuondoshwa kwake kuwekewe utaratibu mzuri ambao utasaidia matumizi yake na faida yake kuingia katika Mfuko wa serikali. Kwa hivyo, niseme tu kwamba wajumbe wetu hawa wa Bodi ya Wazabuni naomba sana wawe watu wenye utaratibu mzuri wa imani kabisa na wawe waadilifu sana katika shughuli zao za kuweka ule usawa unaotakiwa katika mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kunakuwa na *tender* nyingi wakati mwengine, *tender* zetu hizi hutegemea sana watu kutoka katika sehemu mbali mbali.

Mimi ushauri wangu kwa kuwa nchi yetu tunataka kubana matumizi na tunataka kufanya kitu ambacho kibakie mikononi mwetu na pia kiwasaidie wananchi wetu, niiombe wizara kwamba watendaji wetu wa ndani wapewe kipaumbele juu ya maombi yao. Lakini si vyema kuwe na kampuni itoke nje ya nchi iwepo hapa wao ndio wawe kama wale sehemu ya *tender*, wao ndio wanagawa yale mambo mengine yanayopatikana wanachukua wao wanawagaia wazalendo. Hapa kidogo Mheshimiwa, naomba sana suala hili lieleweke kwamba, *tender* zetu wananchi wetu wa ndani wenye makampuni wapewe kipaumbele kwa faida ya nchi yetu. Hii itawasaidia wao na itasaidia mambo mengine katika kuwa karibu na shughuli zetu na mahitaji yetu ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa zaidi ninaloliomba tuna makampuni ambayo wengine hawana vigezo, kwa hivyo, niiombe wizara makampuni haya ambayo yataingia katika *tender* kwa maombi mbali mbali yawe na uwezo na viwango

ambavyo vinakubalika, tusitafute watu tu kwa kuwa makampuni yamo ndani tukasema aa, kampuni yoyote ipewe aa. Viwango ni kitu cha mwanzao kinachokubalika katika mahitaji ya shughuli zetu hizi. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, hili liangaliwe kwa faida ya shughuli zetu hizi ambazo tunaziweka mbele katika kutafuta mapato yetu yaende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilichangia Mswada wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*). Namshukuru sana Mhe. Waziri katika majumuisho yake, wananchi wengi walikuwa hawajaufahamu lakini baada ya kuufahamu wamepata faida, ukimuelimisha mwananchi atafahamu, lakini ukimuondoa tu kama baada ya kumtangazia sheria hajui kitu atapata tabu. Kuna wananchi wengi jana walipongeza sana majumuisho ya Mhe. Waziri wa Fedha, aliposema kwamba kuna asilimia fulani ukimaliza utumishi wako serikalini utapata kiwango fulani, lakini kuna mapungufu fulani haya kwa manufaa yako wewe ya *plan* ya baadae. Kwa hivyo, walikwenda vizuri.

Kwa mswada huu pia namuomba sana Mhe. Waziri, kutoa elimu kwa wananchi, elimu kwa wafanyabiashara na kwa watu wote ni muhimu sana kupewa, ili wajue mswada huu utanufaisha kitu gani. Mimi naamini Mhehsimiwa, huu mswada ni mzuri tena una maelekezo mazuri, unataka kusimamiwa vizuri ili hatma nzuri ipatikane kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu hizi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, elimu ya kutosha itatusaidia na elimu ya kutosha itawapa watu faida ya kujijua tufanye nini ili na sisi tuingie katika mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kuwa mswada huu nimeupitia na nimeona mambo mengi, lakini kubwa ni kuuweka katika sheria nzuri au utaratibu mzuri wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma namba 9 ya mwaka 2005.

Niseme tu kwamba mswada huu ni mzuri na ninauunga mkono kwa asilimia mia moja mimi mwenyewe na wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, naamini kwa kuwa Mwakilishi wao walionichagua hapa hawana wasi wasi na mimi ninaunga mkono na naomba Waheshimiwa wenzangu wauchangie ili kumpa uwezo Mhe. Waziri, auweke vizuri zaidi katika mwelekeo wetu tunaotaka kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono nashukuru.Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, aliyetujaalia tukakutana hapa leo katika Baraza hili tukufu la Wawakilishi kwa

ajili ya kujadili mambo yetu. Tunakuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema utupe uelewa na ufahamu, tunakuomba Mwenyezi Mungu utuongoze katika njia iliyonyooka, *Yarabbi* umpe hekima na busara Rais wetu na viongozi wetu ili waweze kuliongoza taifa letu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo napenda kwanza kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake kwa kuona umuhimu wa kuupeleka mswada huu katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umekuja wakati muwafaka ambapo kumekuwa na kilio cha wananchi juu ya uuzwaji na ununuzi wa mali za umma kama walivyosema wenzangu waliotangulia. Mimi nafikiria au sifikiri naona ndio ilivyo, baada ya kuona haya na wakaona waweke mambo mazuri zaidi kwa ajili ya Wazanzibari wakaona ni bora uletwe mswada huu Barazani ili Wawakilishi tupate kuuchangia, tuushauri na baadae tuelekeze ili mambo yetu yende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mswada huu ulioletwa ambao sisi tunauchangia, hili ni jambo ambalo wenzetu Bara wamekuwa wakilipigia kelele muda mrefu, wamekuwa wakilalamika. Tunaona kwenye Bunge kila mara wanalalamika kuhusu ununuzi na uuzwaji wa mali za umma, mambo kama haya mengi yanazungumzwa. Lakini sisi viongozi wetu wameona ni busara uletwe vizuri na kwa bahati na mimi nimeusoma na nimeuelewa vizuri. Ni mzuri, una kila sifa ya kuufanya tuupitishe.

Kwa upande wangu mimi kabla ya kuendelea na mchango nasema mswada huu nimeuunga mkono kwa asilimia mia moja na ninawaomba wenzangu wote tuunge mkono mswada huu ili tuupitishe iwe sheria na iweze kutumika.

Pia, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi yao kubwa waliyoifanya ya kufanya marekebisho ya baadhi ya maneno na hatimaye tumeona leo hapa katika uwasilishaji wao kumeweza kutengeneza mambo mengi mazuri. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na kamati yake pia nawapa hongera sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala la tathmini ya uwajibikaji ambapo kwa sasa sheria hii ina lengo la kudhibiti matumizi makubwa ya fedha za serikali na kuweka namna bora ya sheria hili ni jambo la msingi, ambalo linatakiwa katika utawala bora kama tunaouzungumza na ndio maana kwa kuzungumzia huo utawala bora mswada huu ndio umeletwa Barazani na hatimaye tukaweza kuuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wamesema maneno mazuri, wametoa michango mizuri, fasaha yenye maslahi ya taifa. Wenzangu walionitangulia mengi wamenifilisi hasa Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame, sasa ukitangulia wewe kuchangia mimi nitakuwa sisemi tena, kwa sababu yale ninayopanga kusema mimi, wewe unayatangulia kuyasema. Sasa mimi siku hizi nataka niwe wa mbele Mheshimiwa ili Mhe. Rashid Makame Shamsi, asinitangulie akawa ananifilisi kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi makubwa kwenye taasisi pamoja na mambo mengine ya uuzaji wa mali za serikali. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, yaani yanaibebesha serikali mzigo, pesa nyingi za serikali zinapotea pale huu ni ukweli na ndio maana tukasema sasa tubadilishe sheria. Sheria zilizopita tuziwache, tupitishe Mswada huu uwe sheria ili tuweze kubana ile mianya yote ya rushwa.

Mhe. Waziri, ahsante sana na timu yako, mimi narudia tena kusema umefanya kazi nzuri, yaani kazi ya kupigiwa mfano na hili sisi Wawakilishi hatuna budi kuliunga mkono kwa nguvu zote.

Lakini pia nilikuwa na jambo moja ambalo nataka kulizungumza jambo ambalo liko kwenye Ibara katika kifungu cha 45 cha Kanuni ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali. Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio penye mtihani ambao nyie mmeuona, kifungu cha (b) kinasema;

"Kuwa na uwazi na uwajibikaji bora bila ya upendeleo"

Mhe. Waziri, hapa ndipo ulipo mshipa wa damu wa matatizo yetu na kwa sababu mmeliona hili, na wenzangu waliotangulia wamelisema, mimi langu ni kutilia mkazo kwamba ili kuliepuka hili na kulifanya hili ambalo tumelizungumza kwenye hichi kifungu cha (b), kwa uwazi uwajibikaji bila ya upendeleo ni lazima tuwe na viongozi waadilifu tusije kufika pahali tukamuonea mtu aibu. Tunapomuona mtu anataka kuchafua, kavunja kuwa muwazi katika kuendeleza mambo haya au kutekeleza wajibu wake huu tusimuonee aibu.

Mhe. Mwenyekiti, tukianza kuja kuwa tutaoneana aibu, hichi kifungu kitakuja kutusuta. Tusikubali kuja tukasutwa na sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe, mtu hawajibike katika idara yake na hawezi kazi, kaonekana kama ana upendeleo fulani kwa sababu anawezekana mtu akaonekana aah, mimi nikitoa tenda hii 10 *percent* yagu itaingia hapa lakini analiangamiza taifa. Mhe

Mwenyekiti, mtu kama huyu hatufai katika nchi hii. Naamini kwa kuyaona haya ambayo mmeyazungumza nyie kwenye hichi kufungu cha 45(b), ndio moja katika sababu kubwa ambayo mmeona kwamba kwa sasa iko haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu, Mzee wetu mzoefu wa Baraza ametoa rai na mimi nakubalina nayo kwamba, ulimwengu wowote au popote wazawa huwa wana nafasi yao. Kwa hiyo, makampuni ya wazalendo katika mambo yetu ni wajibu yakapewa kipaumbele iwapo lakini yanasifa na vigezo vinavyohitajika, sio kwa sababu ni mzalendo, hana sifa, hana uwezo tukalazimisha kama apewa, hapana. Iwapo atakidhi vigezo, yaani atafikia kiwango kinachokubalika wako sawa sawa na makampuni ya kigeni, kampuni ya wazalendo ni vyema zikaangaliwa kwanza. Litatusaidia vipi?

Litatusaidia kuajiri vijana wetu wengi kama ni kwenye kazi, litasaidia kuajiri wataalamu wetu wengi, litatanua wigo wa kupunguza ajira kwa wananchi wetu, tatizo la kuwapa kipaumbele makampuni ya kigeni ni kwamba, kampuni ya kigeni unapoipa nafasi itachukuwa nafasi kubwa ya kuajiri wataalamu kutoka nje.
Lakini unapoiajiri kampuni ya wazalendo kwenye kazi ambazo zinaweza kufanywa na wazawa kama za ujenzi wa barabara, mimi naamini ukiwapa kampuni ya wazawa ikiwa ipo na imekidhi vigezo hawawezi kwenda kumchukua raia kutoka Marekani watamtafuta *resident* injinia mzalendo aliesomea pengine Chuo Kikuu cha Dar-es-Saalam, aliesomea ndani ya nchi yetu au hata awe kasomea nje ya nchi yetu lakini damu ya nchi yake uzalendo bado atakuwa nao. Hili mimi nilikuwa napenda kulizungumza kutia nyama yale maneno aliyozungumza Mwakilishi wa Kijitoupele Mhe. Ali Suleiman (Shihata), kwamba kwenye kutoa nafasi za kampuni kwa kazi mbali mbali za kiserikali makampuni ya wazawa yapewe kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumaliza nilikuwa naomba kutoa kidogo mchango wangu wa masahihisho kwenye kifungu cha 4(2) cha neno "Muhiri" kumeandikwa "Mhuri". Lakini kifungu cha 3 kimesomeka vizuri. Kwa hiyo, ningeomba na hichi kifungu cha 2(a) lile neno "Mhuri" lisomeke kama kilivyosomwa kile kifungu kidogo cha (3) neno "Muhuri" lisiwe "Mhuri. Liko neno 'Muhuri' katika kifungu cha (3).

Pia, nilikuwa napendekeza kitu kimoja katika miswada yetu ni vyema tukatumia sana Kiswahili, tusipende kutumia maneno ya Kiengereza ila pale palipokuwa hapana budi, kwani hivi jamani hatuna neno lililokuwa linatafsirika kinyume na hili neno "*data*" hapa, kwa nini tusitumie neno la Kiswahili, yaani

tusilitafsiri kwa neno la Kiswahili tuendelee kutumia neno '*data'*. Mimi napendekeza kwamba tafsiri za miswada yetu itumike sana kwa maneno ya Kiswahili kwa sababu yatatoa uwelewa hata kwa wananchi wetu kujua nini linalosemwa na nini maudhui ya hili jambo na nini madhumuni yake.

Kwa hiyo, hapa mimi napendekeza hili neno '*data'* liliopo pale kwenye Kifungu cha 6 liweze kutafsiriwa kwa Kiswahili, inawezekana na linalo *translation* yake katika lugha ya Kiswahili, yaani litumike kwa Kiswahili...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, muda wako umekwisha, nakugaiya dakika moja.

Mhe. Omar Seif Abeid: Baada ya haya kuyazungumza ni imani yangu pamoja na Wawakilishi wenzangu na Baraza zima kwa ujumla kwamba, tutauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia ili hatimae uwe sheria na tuweze kuitumia kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Wajumbe niliowatangazieni hapa kwamba atafuatia Mhe. Mmanga, nimuombe kwamba kwa dharura iliyojitokeza atachangia Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, na baadae ataendelea na nafasi yake Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri.Ahsante.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba nichukuwe nafasi hii kwanza kuwapongeza viongozi wote wahusika kwa ajili ya maandalizi ya sheria hii ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa wetu Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia kazi hizi kwa makini, Wizara ya Fedha pamoja na Afisi yao.

Lakini pia nipende kumpongeza pia Katibu Mkuu Kiongozi ndugu Abdulhamid Yahya Mzee kwa kusimamia sana kuhakikisha kwamba pale tunapohitaji sheria zitoke kuzipitisha kwa wakati kwenye gazeti letu la sheria na uchapaji kwa amri ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nipende kusema tu kwamba hii Sheria ya maswala ya manunuzi ni sheria ambayo nadhani kwa wakati huu inafaa na itafanya vizuri na niendelee kuunga mkono na pia kuungana na wenzangu wote wanaunga mkono kwa sababu kuna umuhimu mkubwa ndani yake. Hasa kwanza ukiangalia kwamba mara nyingi tumekuwa tukitaka kuuza vifaa vingi hasa vile

vinavyokuwa vimeharibika kwenye maofisi tunakuwa tunachukuwa utaratibu mwingi tangu unapotaka kuomba mpaka ije iuzwe mpaka ile hali inaharibika kabisa inakuwa haifai tena kwa sababu muda unakuwa mrefu zaidi.

Lakini nimefurahishwa pia na nataka kuwahakikishia wengine wasiwe na wasi wasi na sheria hii ni pamoja katika ukurasa wa 77, kwenye kifungu (a) ambacho kinazungumzia kwamba:

"Katika masuala ya uuzaji hakutakuwa na ubaguzi kuhakikisha usawa, ushindani, uwazi bila ya ubaguzi na thamani ya fedha kwa ununuzi wa ununuzi unaozingatia viwango vya uhalisia"

Mara nyingi wengine wakileta masuala ya kuleta zabuni wanalalamika kwamba, mimi sijui kama nitafikiriwa labda kutakuwa na upendeleo, nataka kuhakikisha kwamba katika suala hili linaonesha wazi kwamba hakutakuwa na masuala ya ubaguzi. Lakini pia katika ukurasa wa 116, kifungu namba 100 ambacho kinasema kwamba:

"Kusimamishwa kwa watoaji wa huduma"

Mhe. Mwenyekiti, katika wasimamizi wa utoaji wa huduma nadhani pia limezingatiwa kwa sababu mara nyingi zinapokuwa zinaanza Zabuni au tenda linapoingia jambo kama kosa moja kwa ajili ya uharibifu au kutofata sheria au utaratibu uliofaa. Ule utekelezaji wa kuja kumaliza lile tatizo mpaka lianze kuendelea tena mchakato unakuwa ni muda mrefu mpaka muda ule unaisha, inakuwa unapoteza muda mwingi na kupoteza imani kwa watu wetu ambayo nadhani pia kwa makosa na adhabu ya Wizara ya Fedha zitaendelea kutolewa taaluma kwa wahusika ambao ni wafanyakazi na wananchi baada ya kungoja mpaka watakapokosa ndio waanze kuelimishwa kwa sababu mara nyingi tumeona kwamba kumekuwa na tabia ya watu kutokupenda kujifunza kisheria mapema mpaka pale tatizo litakapotokezea na sheria mara nyingi inapokuwa umekosea haisemi wewe ulikuwa mjinga hukujua jambo fulani. Kwa hiyo, inakuwa ni tatizo ambalo likifanyiwa mapema na likiandaliwa inakuwa hatuna tatizo sana.

Lakini pia katika ukurasa wa 116 nilipokuwa nasema kwamba, mtoa huduma akisimamishwa na Bodi ya Kitaaluma watoa huduma kwa kosa la kutokuwa na maadili ya kitaaluma. Hapa nataka kusisitiza kusema tu kwamba, katika maisha ni vizuri sana kuwa na maisha yaliyokuwa na maadili ambayo katika ukurasa wa 126 kuhusu msingi wa maadili ni kutafuta njia ya kukuza hadhi ya Serikali ya Zanzibar ndani na nje kulinda kwa kiwango cha uadilidifu wa kazi zote za

taasisi zinazowaajiri, wawe na uwezo wa kiutendaji na elimu ifatwe vizuri kama inavyotakiwa, ni kitu ambacho kinatia moyo kwamba kumbe suala zima la mambo ya uuzaji haya pia yanazingatia suala la uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho, nilikuwa nataka kusema tu kwamba kuna mahala ni kama usahihisho tu ukurasa wa 103, kifungu namba 65, neno "ununuzi" limeandikwa "ununizo" kiasi cha kuhitahi usahihisho tu.

Kwa hayo, machache naamini kabisa kwamba wizara itaendelea kutoa elimu kuhakikisha kwamba yale yote yaliyokusudiwa katika mswada huu yatatekelezwa ipasavyo na kwamba, Ofisi zetu zitafanyakazi kwa utulivu kwa kuamini kabisa kwamba yale tunayokusudia kwenye serikali yetu ili serikali yetu izidi kupewa heshima.

Baada ya kusema hayo Mheshimiwa, napenda niseme tu kwamba naunga mkono asilimia mia moja mswada huu na kuwatakiwa kila la kheri watakaokuwa wanatekeleza. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuuchangia mswada ulio mbele yetu hapa.

Na mimi pia nachukuwa nafasi hii kuzipongeza taasisi zote zilizoshiriki katika kuandaa mswada huu tokea hatua ya awali mpaka kufikia hatua hii ambayo leo hii tunaijadili. Niseme kwamba taasisi hizo zimefanya kazi kubwa na aina yake na hii sehemu iliyobakia ni wajibu wetu sisi Wawakilishi kuukamilisha kwa faida ya jamii yetu yote.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba sheria hii ya manunuzi ina mambo matatu muhimu kwa upande wangu ambayo nataka niyachangie.

Kwanza ni suala la mamlaka yenyewe ya ununuzi na uuzaji wa mali za serikali, lakini pia Bodi ya Zabuni na Kamati na Tathmini. Nichukuwe fursa hii kwa kusema kwamba sheria hii nayo pia imekuja baada ya kutathmini changamoto zinazokubali masuala haya ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali. Lakini msingi zaidi zimekuja katika kudhibiti mapato na matumizi ya serikali. Nilikuwa nikiangalia kwa makini kuhusu kazi ya mamlaka yenyewe lakini pia kazi ya bodi.

Baada ya kutizama kwa makini nimeona kwamba majukumu yake yamepangwa vizuri sana. Lakini suala moja tu ninaloliona ambalo kwa maoni

yangu ndio utakuwa ni upya katika sheria hii, nalo ni suala kwa kiasi gani Wajumbe wa Bodi wataweza kufanikisha majukumu yao, kama Wajumbe wa Bodi hii na nyengine kama hawatobadilika na kufanya kazi kwa mazoea basi mategemeo yetu kwa kweli watakuwa wameyadhoofisha.

Kwa hivyo, mimi nishauri kwamba Wajumbe wa Bodi waachane na utaratibu wa kufanya kazi zao kwa mazoea, kusubiri kumbukumbuku za mkutano katika siku ya mkutano na kurekebisha *comma* na *full stop*, huu si utaratubu mzuri. Lazima Wajumbe wa Bodi wafanye kazi za kujituma, yaani kazi ya kutathmini taasisi wanayoisimamia ili maamuzi yao yawe na ushahidi, kwa utaratibu huu wa mazoea basi hatutofika mbali. Lakini endapo kwamba Wajumbe wa Bodi watafanyakazi kwa njia ya kutafuta taarifa ambazo zitasaidia katika kutoa maamuzi kwa njia hiyo Mhe. Mwenyekiti, tutafika tunakokwenda.

Mara nyingi sana Wajumbe wa Bodi mbali mbali kutokana na kutojituma kutokana na kufanya kazi zao kwa mazoea mara nyingi wanakuwa wanababaishwa na watendaji na kutoa maamuzi ambayo kwa kweli baadae mkija mkiyatathmini mtao kwa kweli mmeendeshwa mchomo. Kwa hivyo, lazima Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka hii wabadilike.

Pia, nikiangalie sifa mbazo mtu atapata sifa ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi, sawa suala la elimu aliyonayo sawa, uzoefu wake sawa. Lakini nadhani si sifa pekee, ni muhimu kuangalia utendaji kwa anaeteuliwa, kujituma kwake. Lakini kubwa zaidi na uzalendo alionao na uwajibikaji wake, haya ni masuala muhimu sana, ukiangalia tu sifa za kitaaluma nadhani itakuwa hatujaitendea haki kwa Wajumbe ambao watakuwa wanafanya kazi katika Bodi kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kwamba ni muhimu sana katika utekelezaji wa Sheria hii kwenye kipengelee hichi cha Bodi ya Zabuni, hii ni muhimu nayo pia inapaswa kufanya kazi kwa ufanisi. Ndiyo maana ule upya utapatikana. Ikiwa watafanya kazi tu kwa mazoea yao, upya hautopatikana na kwa maana hiyo taasisi yenyewe pia ufanisi wake utakuwa ni hafifu. Kwa hivyo, nayo lazima ifanye kazi na lazima ipangwe vizuri.

Jengine ni hizi kamati ambazo zinasaidia katika mchakato wa zabuni ni Kamati ya Tathmini. Hii ni muhimu sana, ni kamati ya msingi na muhimu sana. Inapovuruga na inapoleweshwa kamati hii mara nyingi basi maamuzi yao yanaweza kuwa ni hafifu na yakaweza kuingiza Serikali katika hasara au aibu. Kwa hivyo, mambo hayo kwa kweli ni muhimu kuyazingatia.

Jambo jengine ambalo wenzangu wameligusia na mimi pia ningependa kuligusia sana, sana ni suala hili la *Asset Registration*. Hili katika nyakati hizi kwa kweli, sisi watu wa Serikali bado hatujalitazama kwa ukamilifu wake na uzuri wake. Kwa hivyo, nadhani wakati umefika kwa kila taasisi ya umma kuwa na *asset register* ambalo lina tarifa sahihi na mpya kabisa. Hii inasaidia sana kutunza mali ya Serikali.

Sasa baadhi ya mali inawezekana kuwa hazijulikani kutokana na kukosa na *records* katika madaftari haya. Kuna mali nyengine ni za Serikali lakini zinaonekana kama za watu binafsi kutokana na kuwa hazina kumbukumbu. Kwa hivyo, wakati tukipitisha jambo hili kwenye sheria hii lazima suala la *Asset Registration* tulitie mkazo na ninafikiri itakuwa ni wajibu wa mamlaka kuona kwamba kila Ofisi ya Serikali inakuwa na daftari hili la kumbukumbu ya mali za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nieleze suala jengine kwamba kwamba suala la ununuzi na uuzaji ni muhimu. Lakini ningeomba nafikiri Mhe. Waziri, afikirie suala la kuiongezea kazi mamlaka hii, isiwe ni uuzaji na ununuzi tu, lakini pia suala la utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali litiliwe mkazo na kwa kweli lipewe kazi mamlaka hii kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali. Kama utunzaji utakuwa hafifu hicho cha kuuza hakitopatikana. Kwa hivyo, suala hili nalo namuomba Mhe. Waziri, aliangalie kwa umakini sana.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri kwamba tujenge jamii yenye kuheshimu maadili ya ununuzi, uuzaji na utunzaji wa mali za umma. Jambo hili linaonekana kwa sasa kushuka kidogo kwa kweli. Maadili yetu ya kuheshimu mali za umma yameshuka na wakati mwengine tunasema yamepotea. Na hii inatokana katika ngazi zote. Ngazi hata za raia wa kawaida, ngazi za wafanyakazi na hata ngazi ya baadhi ya viongozi kwa utunzaji wa mali za umma umeshuka. Kwa hivyo, imefika wakati tuyajenge maadili ya kuheshimu mali za umma. Na mali za umma ni mali za umma, kwa hivyo, zinanufaisha umme, hivyo, lazima tuzitunze kwa nguvu zote.

Mwisho kabisa, niseme kwamba ninaunga mkono sheria hii na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkoani, kuanzia Kisiwa Panza kwa upande wa Kusini mpaka Makombeni kwa upande wa Kaskazini tunaunga mkono sheria hii.
Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mhe. Said Soud Said, ili na yeye aweze kuchangia na baadae atafuatia Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Manunuzi.

Kwa kweli Mswada huu umeletwa wakati muafaka, wakati ambapo sasa Zanzibar inapiga hatua ya mabadiliko makubwa ya kiutawala. Mhe. Mwenyekiti, awamu iliyopita kulikuwa na watu Zanzibar waliifanya kama shamba la bibi. Walikuwa na uwezo wa kuuza mali za Serikali bila hata ya ushauri, bila hata Bodi, bila hata minada. Bali mtu alikuwa anaandikiwa tu akifika anachukua basi.

Katika mazingatio ya Serikali hivi sasa wameona kuna haja ya kuweka Mswada wa Sheria hii ili wananchi wa Zanzibar waweze kupata haki sawa za ushindani juu ya unununzi. Yaani Mswada huu umetayarishwa na Wizara inayohusika kwa utaalamu wa hali ya juu wenye nguvu za kutetea hoja, wenye nguvu za kuangalia mali za Serikali hazipotei bure na pia Wazalendo wenye kuumwa na mali za umma zisipotee bure.

Kwa hivyo, Mswada huu ni Mswada ambao unatuweka sisi Wazanzibari kupata haki sawa katika hoja nzima ya manunuzi. Utakwenda kwenye ushindani, utatia bei yako na ikiwa ndogo una haki ya kuongeza mpaka kufikia hatua ya kwamba wewe sasa ni mnunuzi na Serikali itakuuzia. Lakini ule utaratibu wa kuuziana *under table*, ule utakuwa haupo kwa sababu ulikuwa unajenga misingi ya rushwa, misingi ya kuonekana huyu bora, huyu si bora.

Lakini kimsingi katika kutengeneza sheria hii, Serikali imeona ni vyema sasa tukatumia nafasi ya kuipatia Serikali mapato. Kwa sababu ushindani huu utaongeza mapato kwenye Serikali na ndiyo maana tukawa tayari sisi Serikali kusema kwamba Mswada huu sasa upelekwe kwenye Baraza la Wawakilishi na upitishwe ili Serikali isikose mapato. Kwa sababu kitu cha milioni moja basi kilikuwa kinauzwa laki moja na nusu, kitu cha milioni hamsini kilikuwa kinauzwa milioni mbili na nusu na milioni tatu kwa kujuana.

Lakini ndani ya mfumo huu wa Bodi, mfumo huu wa mauzaji, mfumo huu uliotengenezwa, Serikali itapata mapato yake kama kawaida. Na ninaamni kabisa kwamba ile dhana ya kwamba labda mimi mjomba wangu Waziri, kama yangu Waziri basi wacha nipite chini ya meza nikanunue kitu kile cha Serikali kwa bei mbovu, haipo tena hiyo.

Kwa hivyo, Wazanzibari wajivune, Wazanzibari watumie nafasi nayo na wa-*support* Mswada huu wote; Wawakilishi wote ninawaomba wa-*support*

Mswada huu wote ili upite kwa madhumuni ya kuondoa ile dhana ya rushwa iliyokuwa ikitawala hapo nyuma ya watu kuuziana vitu vya Serikali kwa bei poa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein akisaidiwa na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi pamoja na Mawaziri wake wote, pamoja na Wawakilishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tumefurahi sana kuona kwamba kila kilichokuwa kinakwaza kinaletwa mbele ya Baraza la Wawakilishi na kinatungiwa sheria ili kwa matumizi halali ya nchi yetu. (*Makofi*)

Kwa vile Wawakilishi Mswada huu ni Mswada ambao unawaondolea manung'uniko waliotupigia kura, Mswada ambao utawajengea nguvu waliotupigia kura ili kuona kwamba hakuna kinafanyika tena sasa kwa njia za panya kwa lugha nyengine. Hivyo, tunaondoa dhana ya njia za panya na tunawataka Wazanzibari wote waamini kwamba sasa Serikali yao ipo pamoja nao na itawafanyia kila linalostahiki ili wapate haki sawa. Na ninaamini Wawakilishi sisi tutakuwa tayari kutoa ujumbe kwa wananchi wetu wote Unguja na Pemba kwamba, waachane na ile dhana ya kupokea manung'uniko na maneno yaliyokuwa yanakaa kwenye vijiwe na mizizi ya miembe dhidi ya Serikali. Sisi sote tuwe tayari kupambana na watu hao ili Serikali yetu iendelee kufanya mambo yanayostahiki kwa mujibu wa Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Sisi sote ni walinzi wa Mswada huu, sisi sote tunastahiki kuunga mkono Mswada huu na pia kuufanyia kazi, na kwa sababu sheria zimejitangaza wazi wazi kwamba, yeyote atakayekiuka Mswada huu taratibu za kisheria zitambana. Kwa vile hakuna haja ya kuambizana chini ya miti, chini ya vigogo. Unaliona jambo limekwenda ovyo halistahili unayo haki kama Mwakilishi, unayo haki kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuleta hoja yako kwa njia za taratibu ili mauzo na manunuzi yawe yanakwenda vile ambavyo tumekubaliana humu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu mimi naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na ninawaomba Wawakilishi wenzangu tuunge mkono Mswada huu kwa asilimia mia kwa mia ili tuweze kufanya ule wajibu uliotuleta hapa ndani ya ukumbi huu hii leo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said, kwa mchango wako na kuwaomba Wajumbe waupitishe, nina imani kwamba wataupitisha. Kwa sasa mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Manunuzi, mimi ninazungumza kwa ujumla wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii kwa kutuletea kitu hichi kizuri sana. Lakini pia nichukue nafasi ya kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa sehemu kubwa ya marekebisho, lakini na kunishirikisha kama sehemu ya mdau; maoni mengi nikwenda kuchangia kule lakini leo najalizia tu kidogo. Kuna maeneo nimeona bora nisimame nikazie kazie, lakini sehemu kubwa ya yale maoni yetu ambayo walinishirikisha kupitia Kamati yao niliyapeleka kule. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nende tu moja kwa moja katika Kifungu cha 39, ambacho kinaelezea;

> "Tathmini zote za zabuni lazima zifanywe na Kamati ya Tathmini ambayo itatoa taarifa katika Kitengo cha Manunuzi na Uuzaji wa mali za Serikali".

Mhe. Mwenyekiti, niende tu katika Kifungu cha 39(2)(c), kinasema;

> "Kuangalia uwezo wa mzabuni kwa kutekeleza mkataba wa zabuni".

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi naomba nizungumzie kidogo ili tutakapokwenda kwenye kutengeneza kanuni, maana hapa tupo katika sheria, kuna kanuni mbele yake ambayo Mhe. Waziri ataiandaa.

Hapa katika kuangalia uwezo wa mzabuni hasa katika *international tender*. Ninazungumza zile *tenders* za kuwashirikisha wale wazabuni wakubwa. Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo hapa tunalikosa kulifanyia kazi kwa ufanisi zaidi na hasa pale ambapo wale wazabuni wakubwa wanapotuletea taarifa zao za uwezo wao wa kifedha. Wanatuletea taarifa kupitia mabenki ya nje na ninazungumzia *bill bonds* zile ambazo zinakuwa ni sehemu ya kwenda kupima ile *performance* yake. Sasa wakituletea *bill bonds* zile kutoka katika mabenki ya nje, tunakuwa tuna nafasi ndogo sana ya Kamati ya Tathmini kuwa na uwezo wa kwenda ku

zitambua au kuzihakiki. Ijapokuwa kuna eneo la *juridice*, lakini nizungumze kwa ujumla wake wa Kamati ya Tathmini pale ambapo inafanya kazi zake kwa kipengele hichi, tunakosa ufanisi wa moja kwa moja.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri katika kuja kutengeneza kanuni kuwe kuna kipengele ambacho eneo hili la kukagua hizi *bill bonds* au *bill security* ambazo zitakuwa zinazungumzia hasa suala la fedha au uwezo wa kifedha kwa yale makampuni ya nje au wazabuni wa nje ambao tunataka kuingia nao mikataba katika kufanya kazi zetu za ndani, basi benki zetu za ndani zitumike katika kuhakiki taarifa zao za kifedha.

Pasi na kufanya hivyo kwa kutumia tu Kamati ya Tathmini hatuwezi kuisaidia nchi, tunaweza kuingia katika mikataba na mtu ambaye kaainisha tu *bill bond* yake katika *document* ya tenda yake ambayo katupa sisi, na Kamati ya *Evaluation* wanaangalia hii imetoka katika benki fulani mfano China, Korea au nchi nyengine kwa wale wazabuni ambao watatoka nje ya nchi. Tutaangalia juu juu uwezo wake wa kifedha lakini lile fungu hasa na tathmini ya ndani hatuwezi kuipata.

Mhe. Mwenyekiti, Sasa ninasema katika eneo hili la Kifungu cha (c) kwenye kuliwekea ubora zaidi katika utungaji wa kanuni zetu, basi tuje tuzingatie itakapofika wakati wa kuangalia zile *bill bonds*, basi tuwe tunawashirikisha benki za ndani ambazo kama *PBZ* ili kuweza kumtambua kwa uwezo wa kifedha yule. Baada ya ile *document* yake ya aina hiyo ambayo nimeitaja tumeikagua basi Kamati ya Tathmini iendelee na kazi.

Lakini katika eneo hilo hilo Kifungu cha 2 (e), kinasema;

"Kuwasilisha taarifa ya tathmini kwa Kitengo cha Manunuzi".

Mhe. Mwenyekiti, Kama tukiangalia uzuri katika majukumu ya *Tender Board* inachagua hii Kamati ya Tathmini. Ninaelewa Kamati ya Tathmini kazi zake na ndiyo maana nikasema katika eneo hili pana mapungufu kidogo tu na siyo sana, na naomba nifanye marekebisho kwa yale maoni yangu ambayo ninahisi yanaweza yakasaidia eneo hili.

Isomeke kama hivi; "Kuwasilisha ripoti ya tathmini", iondoke Kitengo cha Manunuzi, irejee tena kwa Bodi ya Wazabuni kwa sababu ndiyo iliyoagiza kufanya kazi ya tathmini, siyo Kitengo cha Manunuzi. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hapa, kwa sababu kazi waliofanya hawa inatoka kwenye Bodi ya Wazabuni na Bodi ya Wazabuni ndiyo yenye uwezo wa

kuichagua timu hii ya *evaluation* baada ya pale mwanzo Kitengo hichi cha Manunuzi 'ku-*propose* kwa Bodi ya Wazabuni na Bodi ya Wazabuni inathibitisha uwepo wa Kamati ya Tathmini kwa kazi maalum'. Kwa hivyo, naomba iwe 'kuwasilisha ripoti na siyo taarifa, isomeke "Kuwasilisha ripoti ya tathmini kwa Bodi ya Wazabuni", kwa sababu ndiyo iliyotoa kazi yenyewe.(*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba tena nijazie katika eneo la Kifungu cha 39(5) kinasema;

"Wajumbe wanatakiwa wawe katika kiwango cha juu".

Naomba ufafanuzi kwa sababu kiwango cha juu na uzoefu. Kiwango cha juu gani Mhe. Waziri? Sasa ni lazima tutoe tafsiri ya kiwango cha juu hichi, ni kiwango kipi. Kwa sababu Kifungu namba (5), nimekisoma hapo lakini naomba nikirejee, kinasema;

"Wajumbe wanatakiwa wawe katika kiwango cha juu".

Mhe. Mwenyekiti, Kiwango cha juu kipi; cha elimu au?

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi kwa Mhe. Waziri, atakapokuja katika eneo hilo tunahitaji hichi kiwango cha juu kiwe kipi, isijekuwa kiwango cha juu watu wakatafsiri vyengine, ikiwa cha unene labda.(*Makafi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba Kifungu cha 64, ambacho kinazungumzia;

"Utaratibu wote wa wazabuni utajumuisha utaratibu wa kupokea...", neno kidogo limekosekana hapo, limekuwa "kupekea", "...lakini iwe kupokea na kufungua zabuni kuliko rasmi".

Mhe. Mwenyekiti, Hii lugha ya ufunguzi wa zabuni, siku ya ufunguzi wa zabuni ile mara nyingi utaratibu wetu ambao tunatoka nao huko nyuma na ninapenda sana na hapa tufanye marekebisho kidogo, kwa sababu nahisi kwangu haikukaa sawa. Lakini pale ambapo Mhe. Waziri, unaweza ukaja ukanipa ufafanuzi wa ziada na ninaweza nikakubaliana nayo.

Lakini mimi nahisi parekebishwe hayo na isomeke;

"Utaratibu wote wa zabuni utajumuisha utaratibu wa kupokea na kufungua zabuni kwa kuwashirikisha wazabuni".

Naomba isomeke hivyo kwa sababu hapa ilipo haina lugha. Siku ya ufunguzi wa zabuni yenyewe kuwashirikisha wazabuni alau kujua zile *documents* kweli kama ziliambiwa ziwepo *sealed,* zitakuwa *sealed.* Lakini hii lugha haiji katika ule ufafanuzi wa ziada kama kweli tutawashirikisha. Sasa isomeke vizuri kama hivyo ambavyo nimeifanyia marekebisho.

Lakini pia naomba niende Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 90, "Aina za mikataba". Zimeainishwa hapo 90 (2) aina za mikataba zipo karibu nane. Lakini aina hizi zipo kwa ujumla wake, hazikutoa tafsiri kwamba, mkataba wa malipo wa awamu utakuwa tafsiri yake ni ipi, mkataba wa malipo mfano ya asilimia kwa zile tafsiri zake. Sasa nilikuwa naomba eneo hili la mikataba lipo vizuri alau tuzidishe kifungu kwa tafsiri ya mikataba hii itapatikana kwenye kanuni ambayo pengine itatungwa kufuatana na sheria hii. Sasa alau tuone tu hapa tume-*list,* lakini ile tafsiri yake ipo wapi. Sasa tusije tukatumia vibaya matumizi ya sheria hii yakaja yakatuhukumu badala ya kutusaidia. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kumshukuru zaidi Mhe. Waziri na Katibu Mkuu na Kamati na Wajumbe wote ambao wamefanya kazi hii ya ziada.

Mimi mchango wangu kwa leo utakuwa mfupi kwa sababu sehemu kubwa ya wadau nilishirikishwa na siku mbili hizi tulipata nafasi ya kusaidia, lakini maeneo hayo niliona pia niyasemee.

Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwakilishi. Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa katika meza yangu hakuna mchangiaji mwengine hadi sasa na kwa kuwa muda wetu uliobaki Waziri hawezi kuutumia kwa kuweza kujibu hoja hizi, nitamuomba Mheshimiwa. Muda uliobakia ni dakika ishirini, kwa hivyo, tunaweza tukaahirisha bila ya kutengua Kanuni ya muda.

Ninachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote kwa michango yenu na tujitayarishe kumpa nafasi Mhe. Waziri, aweze kuja kuweka sawa Mswada wetu huu wakati wa jioni. Kwa hivyo, mjadala huu ninaufunga hakutakuwa na mjadala mwengine wa kuchangia wakati wa jioni. Naomba kuliahirisha Baraza hili hadi huo muda wa saa kumi na moja jioni. Ahsanteni.

(Saa 6.40 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, kwa kutujaalia uzima na afya na kutuwezesha kukutana tena hapa kuendelea na mijadala yetu katika kikao hiki.

Pia, nichukuwe fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kukushukuru wewe binafsi, kwa jinsi ulivyosimamia mijadala wakati wa asubuhi, mijadala iliyohusu Mswada wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nirudie kuwashukuru sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Nimshukuru sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid, kwa kuwasilisha maoni ya kamati vizuri. Nimueleze kwamba maoni ya kamati yamezingatiwa kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia na ambao hawakupata fursa ya kuchangia, na kwamba naamini wote kabisa wataiunga mkono hoja hii, na kwa namna hiyo Baraza kwa ujumla wetu tutaupitisha mswada wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mswada ulichangiwa na wajumbe 13, nawashukuru na kuwapongeza wote kwa michango mizuri na maelezo mazuri. Lakini naomba niwatambuwe kwa kuwataja wale wote waliochangia kama ifuatavyo.

1. Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei), kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambaye pia ni Mjumbe wa Baraza hili kwa kupitia Jimbo la Wawi.
2. Mhe. Machano Othman Said
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Dk. Makame Ali Ussi
5. Mhe. Ali Suleiman Ali
6. Mhe. Omar Seif Abeid
7. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
8. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

9. Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
10. Mhe. Miraji Khamis Mussa

Mhe. Mwenyekiti, na wajumbe waliochangia kwa maandishi ni;

11. Mhe. Shehe Hamad Mattar
12. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na
13. Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa ufafanuzi na maelezo kuhusiana na hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo. Kwanza nianze na Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Machano Othman Said, kwa kutoa ufafanuzi wa kina kwenye mswada huu wa sheria. Vile vile, alitaka kwenye maeneo fulani kupata ufafanuzi na hasa alitaka kuwepo kiwango maalum cha zabuni kwa wazabuni wa ndani, kwamba kiwango hicho kiwekwe kwa ajili ya wazabuni wa ndani.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili pia lilishauriwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Omar Seif Bakar. Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba kuna utaratibu maalum umewekwa ndani ya mswada wa sheria hii, kwa ajili ya kutoa upendeleo maalum kwa wazabuni wa ndani. Sheria ya sasa namba 9 ya mwaka 2005 haikuwa na utaratibu huo. Lakini mswada huu ambao tunaupendekeza basi utaratibu huo umewekwa.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wasome tafsiri iliyorekebishwa na kamati, kamati imeweka wazi kabisa ni nani hao wazabuni wa ndani. Lakini vile vile ukitizama jadweli namba 5 pale utakuta kuna viwango mbali mbali, kuna viwango kwa bidhaa, kazi kwa maana *civil work* na pia viwango kwa ushauri elekezi, yaani huduma za ushauri elekezi.

Kwa mara ya mwanzo tumetoa upendeleo maalum kwa wazabuni wa ndani, kwa maana ya bidhaa kwa mfano, bidhaa zenye thamani mpaka shilingi milioni 600 hizo hawatoruhusiwa wazabuni wa nje, zitakuwa ni kwa wazabuni wa ndani, zamani utaratibu huo haukuwepo. Wazabuni wa nje wataanza kuingia kwenye ushindani wa bidhaa iwapo thamani itazidi shilingi milioni 600.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kazi kiwango kilichowekwa kwa wazabuni wa ndani ni mpaka shilingi bilioni mbili, hizo ni kwa wazabuni wa ndani,

wazabuni wa nje hawatoruhusika. Lakini vile vile kwa huduma za ushauri elekezi kumewekwa kiwango mpaka shilingi milioni 500, wazabuni wa nje hawataruhusiwa. Hata kwa vile viwango vya wazabuni wa nje bado Mhe. Mwenyekiti, wazabuni wa ndani wanaruhusika kuingia, na iwapo kama kuna tofauti ya bei kwenye ushindani, baina ya mzabuni wa ndani na mzabuni wa nje, itakuwa ni kati ya asilimia 10 na asilimia 15, bado sheria inataka kazi hiyo apewe mzabuni wa ndani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ni jukumu la wazabuni wetu wa ndani na wananchi kwa ujumla, kwanza kuielewa hii sheria na fursa zilizopo. Vile vile, wazabuni wa ndani wajitayarishe, kwa sababu watahitaji kuwa na viwango, waweze kupita kwenye *technical evaluation* na *finance evaluation*, kwa zile zabuni za nje ambazo zitawashirikisha wazabuni wa nje. Maana yake wao watapewa upendeleo wa asilimia 10 mpaka 15 ya tofauti ya bei, iwapo watafikia vigezo vinavyohitajika vya kiufundi na vile vile na vya kibei. Kwa hivyo, hapo tutaiona wazi kwamba sheria hii imetoa upendeleo maalum sana kwa wazabuni wetu wa ndani.

Mhe. Machano Othman Said, pia, alizungumzia kuhusiana na suala la Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwemo katika bodi mbali mbali. Suala hili kama alivyosema yeye mwenyewe Mhe. Mwenyekiti lilikuwepo, ulikuwepo utaratibu huu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pia kuwemo katika bodi mbali mbali. Lakini kwa suala zima la msingi wa utawala bora, ilionekana si busara Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa pia wajumbe wa bodi.

Sababu yake ni kwamba chombo hiki ni chombo cha usimamizi, kinafanyakazi ya *oversight function* ndio kazi yake na ndio jukumu lake Baraza la Wawakilishi. Sasa wakiingia kwenye bodi itakuwa wajumbe wanajiingiza moja kwa moja kwenye shughuli za uendeshaji, kutakuwa na *conflicts.* Huku wewe unaendesha na huku wewe ni msimamizi hayawezi kwenda mambo haya pamoja. Kwa hivyo, busara hiyo iliyotumika ndio maana sheria za sasa hivi haziwatambui Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa wajumbe wa bodi.

Pia, Mhe. Machano Othman Said, alisema suala la kuwepo kwa bei kubwa kwa bidhaa zinazopitia katika zabuni kuliko bei halisi. Ni kweli suala hili lipo, na hata sisi tunaliona bado ni changamoto. Kwa sababu yapo mambo mengi, wanapoweka hawa wenzetu bei ndani ya ushindani wanaangalia mambo mengi, kuna gharama za kujiandaa, zile gharama za maandalizi pia wanaziweka kule,

na wakati mwengine hutokezea kucheleweshwa malipo wanaziweka katika bei zao, kwa hivyo, mara nyingi zinakuwa juu kuliko bei halisi.

Mhe. Mwenyekiti, ushindani unawekwa kwa sababu ya kuangalia ile *market value*, yaani bei halisi, haiwezi kuwa sawa sawa, lakini angalau inayokaribia bei halisi ndio maana ya ushindani. Lakini wazo hili tumelichukua na tutalifanyia kazi kwenye kanuni, nadhani ni busara kuweka pia *range* ambayo tunaweza tukaikubali zabuni hiyo. Sasa nalo tunaliangalia tutaweza kufikiria kuwa na *range* kwamba ikipindukia kiasi hiki au asilimia hii ya bei, basi labda tenda hiyo isitishwe na irudiwe tena, hilo tutalifanyia kazi na tutaliangalia kwa umakini sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Rashid, kama ilivyokuwa kawaida yake amechangia vizuri sana, na inaonesha wazi kwamba Mhe. Mjumbe, aliufanyia haki mswada huu, kwa maana aliupitia kipengele kwa kipengele na ndio maana akagundua maeneo mengi ambayo yalihitaji marekebisho. Nimueleze tu mengi ya yale aliyoyagundua kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo tayari walikwishayaona na tayari yalikwishafanyiwa masahihisho au marekebisho.

Mhe. Spika, lakini kuna suala la bodi kufanya uamuzi bila ya kushirikisha wataalamu, suala hili alilizungumza na ni muhimu sana. Hatuwezi tukawa na wajumbe wa bodi ambao watakuwa na taaluma zote zitakazohitajika katika manunuzi ya bidhaa, kazi au manunuzi ya ushauri elekezi sio rahisi. Ndio maana kazi hii ya kuingiza wataalamu imewekwa kwenye kamati ya tathmini ile *evaluation team* au *evaluation committee.* Sasa pale imetolewa fursa kuchaguliwa wajumbe ambao watakuwa na taaluma katika suala lile linalozungumzwa ndio wataingia kwenye *evaluation committee*. Mapendekezo yanayotoka kwenye hii Kamati ya Tathmini ndio yanayopelekwa kwenye bodi kwa ajili ya kuzingatiwa na kufanyiwa maamuzi, ni suala zuri, lakini ndani ya sheria inayopendekezwa limewekewa utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Dk. Makame Ali Ussi, alizungumzia sifa za wajumbe wa bodi na pia, Mhe. Miraji Khamis Mussa na yeye alizungumzia suala hili. Lakini kwenye sifa za wajumbe wa bodi nieleze kwamba utaratibu unaopendekezwa kuwa na wajumbe watatu, pamoja na Mwenyekiti ambapo hawa watakuwa ni Wakuu wa Idara ya Wizara inayohusika na hawa wote wanne ni wateuliwa kwa Mhe. Rais mwenyewe katika wizara ile inayohusika. Kwa hivyo, tunatarajia hawa kwamba ni watu makini, wataalamu na wameonekana kuwa na vigezo na sifa zinazohitajika kwa kazi wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, pia bodi itakuwa na wajumbe wawili kutoka kwenye ile wizara husika, ambapo wajumbe hawa watakuwa ni maafisa waandamizi, yaani *senior officers* katika wizara ile, sheria imeweka wazi ndio kiwango ambacho kinakusudiwa. Lakini na mjumbe mmoja atatoka Wizara ya Fedha na Mipango ambaye na yeye atakuwa ni *officer* muandamizi. Kwa hivyo, hili tusiwe na wasi wasi, wajumbe wa bodi watakuwa na sifa zinazohitajika na zimewekwa ndani ya mswada wa sheria unaopendekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine lilizungumzwa la viwango ambalo alilizungumza Mhe. Miraji Khamis Mussa, ambalo lilikuwa katika kifungu cha 39(5). Pia, nimuombe Mhe. Miraji Khamis, asome ripoti ya kamati tayari imeshalifanyia masahihisho kwenye ukurasa wa 16.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Ali Ussi, pia alizungumzia suala la utiaji thamani, kwa maana ya *valuation* na alizungumzia masuala ya *depreciation* kwa kutumia *straight-line method.* Lakini nimueleze tu kwamba hata tukitumia *depreciation* kwa kutumia *straight-line method* bado *value* ya ile *asset* haitokuwa *zero,* kutakuweko na *solvent value*. Lakini pamoja na hayo ushauri wake huu ni muhimu sana, Mhe. Mwenyekiti, sisi tunauchukua, kwa maana ya kwamba mbali ya kufanya *valuation* ya mwanzo wakati wa kuuza, lakini kabla ya kuuza tunaweza pia tukaweka utaratibu wa kuweka *revaluation,* yaani kutathmini kwa mara ya pili ili kuhakikisha kwamba *assets* zetu hazipotei na zinapata bei ya soko.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Dk. Makame, alizungumzia suala la kuwa na *asset register*, ni suala muhimu. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, tunalipokea na tunalichukua, tunahakikisha pale ambapo halijafanyiwa kazi vizuri basi linafanyiwa kazi vizuri katika taasisi zetu.

Vile vile, suala la *asset register* pia lilizungumzwa na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri. Kwa hivyo, hili nalo namueleza kwamba tunalichukua ni jambo zuri, kwa kweli ni lazima tuhakikishe kwamba *assets* zote zimekuwa *registered* vizuri, na kila mara tunafanya *update* ya *register* ili kuona hali halisi ya *assets* za serikali na jinsi zinavyotumika.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), alizungumzia kuhusu bodi iundwe na watu waadilifu. Nakubaliana naye na suala hili pia liligusiwa sana na Mhe. Said Soud na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Tunaweza kuwa na sheria nzuri, lakini bila ya kuwa na wajumbe waadilifu hatutoweza kufanikiwa, nakubaliana nao mia kwa mia,

uadilifu ndio jambo la kwanza kabisa. Ndio maana ndani ya sheria hii kuna sehemu nitaielezea imeweka wazi kabisa ndani ya Kanuni za Sheria ya ununuzi, misingi, yaani *principles* katika masuala ya ununuzi.

Mhe. Ali Suleiman, pia, alizungumzia suala la makampuni yasiyokuwa na uwezo na viwango. Ndani ya Mswada wa sheria hii tumeweka tathmini mbili kufanyika; Moja tunaita tathmini ya awali, kwa maana ya *prequalification*, ambapo hapa zabuni inafanyiwa tathmini ya ile *technical specifications* zake, yaani ile tathmini ya kitaalamu. Lakini pia tathmini ya bei, wale watakaokuwa hawakufikia viwango wanatolewa kabla ya kuanza mchakato wenyewe wa tathmini. Lakini hata tukishampata mzabuni kwa kupitia sheria hii tunayopendekeza, basi kuna *postqualification*, kwa maana ya tathmini ya mwisho, na tathmini ya mwisho anafanyiwa yule aliyeshinda nafasi ya kwanza kwa kutembelewa kwenye *site* yake ili tujiridhishe kwamba yale aliyoyazungumza kwenye *tender document* yake au nyaraka zake za zabuni kwamba ni sahihi. Kama atasema alijenga mahala, basi panafuatiliwa hapo alipojenga na kuona ubora wa hilo jengo alilojenga.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala hili tusiwe na wasi wasi sheria imeweka. Lakini suala zima la uadilifu bado linarudi hapa, kwa sababu hawa wanaokwenda kumfanyia *post qualification* lazima wawe ni watu waadilifu, wasirudishe ripoti ya uongo. Kwa hivyo, suala la uadilifu lakini pia ni suala la kufuata sheria yenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sheria hii iko vizuri, utaratibu uko wazi, lakini uadilifu ni jambo la muhimu.

Mhe. Ali Suleimani Ali, vile vile, alizungumzia suala la taaluma kwa wazabuni wa ndani hasa na wananchi kwa ujumla. Suala hili linawekewa utaratibu wa kutoa taaluma hiyo, lakini hata kwenye sheria hii yalikuwa yanatolewa mafunzo mbali mbali. Lakini la kusikitisha ni kwamba mialiko inapotolewa kwa wazabuni mbali mbali, wale wamiliki wenyewe sio wanaoshiriki kwenye semina hizo au kwenye warsha hizo. Sasa hapa tuwaombe wananchi na hasa wazabuni wa ndani. Inapotolewa mialiko ya kuwalikwa kuja kwenye mafunzo basi waje wao wenyewe wasitume wale *staff* wao wa chini.

Suala la taaluma pia Mhe. Shamata, alilizungumza na naomba achukue hayo kama ndio maelezo ya hoja hii.

Mhe. Omar Seif Abeid, nae amehimiza suala la uwazi, uadilifu ambao kama nilivyosema Mhe. Maudlin Castico, Mhe. Said Sudi, Mhe. Ali Suleiman na Mhe. Mmanga Mjengo, wote walizungumza suala la uadilifu, na kwenye hili tayari nimeshazungumza kwamba ndani ya sheria katika Sehemu ya Nne ya

sheria hii ambayo inazungumzia Kanuni za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, kumewekwa misingi kwa maana ya *principles* na hizo naomba kuzitaja Mhe. Mwenyekiti.

1. Msingi wa mwano ni kuondokana na ubaguzi wa aina yoyote ile katika masuala ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Serikali.

2. Suala la uwazi, uwajibikaji na bila ya kuwa na upendeleo wowote.

3. Kuwepo ushindani na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana *value for money*.

4. Kuwepo usiri, watendaji wetu lazima wahakikishe wanaweka usiri kabisa wa zabuni zinazotolewa na wazabuni mbali mbali.

5. Kuzingatia uchumi na uwajibikaji.

6. Kuimarisha uadilifu na uaminifu.

Kwa ndani ya misingi ya Kanuni za sheria hii, masuala haya ya uadilifu na uaminifu yamewekwa wazi kabisa.

Kuna suala pia la Mhe. Omar Seif Abeid, la masahihisho ya maandishi hilo nae nimueleze kwamba tayari limeshafanyiwa kazi na Kamati, na hivi sasa kamati ukisoma taarifa ya kamati utagundua maeneo mengi yaliyokuwa na matatizo yamerekebishwa.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili kupewa kipaumbele tumelipokea na kila pale itakapowezekana kutumia neno la Kiswahili basi litatumika neno la Kiswahili.

Mhe. Maudline Cyrus Castico, alizungumzia masuala ya maadili na ubaguzi na uwazi tayari nimeshalitolea maelezo.

Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, amehimiza kamati ya tathmini, nimeshalieleza hili kwamba Kamati ya tathmini ni muhimu sana, na nimeeleza kwamba baadhi ya wajumbe wake wanakuwa ni wale watu ambao wana taaluma katika yale manunuzi yanayotakiwa kufanywa. Lakini *asset register* tayari nimeshalizungumza na bodi tayari nimeshaizungumza, sasa kuhimiza hapa uadilifu, utendaji na uwajibikaji, hili tunalichukua na wakati wa utekelezaji wa sheria hii, ikipitishwa basi tutahakikisha tunatoa taaluma kwa upana wake na

kuhakikisha tunasimamia kwa ukamilifu ili kusitokee mianya ambayo itaweza kupoteza fedha za umma.

Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, pia, alizungumzia kuhusu mamlaka kupewa jukumu la utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, hapa naomba kueleza kwamba Mamlaka ina jukumu la msingi la usimamizi kwa maana ya *Regulation*, kwa hivyo, Mamlaka kwa mujibu wa Sheria inayopendekezwa ni *Regulator*, kwa hivyo, hatupaswi kumpa kazi nyengine yeye *Regulator*, lakini wakati huo huo Mamlaka itakuwa na jukumu la kupokea mlalamiko kwa maana ya *Pearland Authority*. Sasa tumpe jukumu la *Regulation* na pia la kupokea malalamiko, lakini masuala mengine ya uhifadhi wa taarifa bado yabaki kwenye Idara ile ya Mitaji ya umma kwa maana ya *Public Investment*.

Ndani ya Sheria hii mitaji ya umma na manunuzi yako chini ya Idara moja, sasa ikipita sheria hii tunatenganisha majukumu haya, masuala ya hifadhi za taarifa na kumbukumbu zitabaki kwa *Public Investment Department* na hili suala la *Regulation* pamoja na kupokea malalamiko litabaki kwa chombo hichi ambacho kitaanzishwa na sheria hii.

Nampongeza sana Mhe. Said Sudi, amenisaidia sana kuweka sawa mambo na kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe ili wazidi kuelewa Mswada wa Sheria hii, na kwa namna hiyo naomba nisimjibu kitu kwa sababu alinisaidia kazi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa, kwanza nampongeza sana na yeye alipata nafasi nzuri ya kupitia Mswada huu, ameingia ndani amegundua dosari nyingi ambazo kwa bahati nzuri tayari zimeshafanyiwa kazi na Kamati, lakini alizungumzia suala jengine muhimu sana la uwezo wa mdhabuni kwa maana ya kuwa na *Security Bond* dhamana, alitaka kwamba zitumike benki zetu kwa ajili ya kufuatilia. Niseme tu kwamba ni suala muhimu na ushauri huu tunaupokea na tutaufanyia kazi vile itakavyostahiki basi tutauweka katika Kanuni za sheria hii.

Lakini pia alizungumzia Wajumbe wa Bodi wawe katika kiwango cha juu, hili tayari nimeshalitolea ufafanuzi, alizungumzia kuhusiana na kifungu cha 64, kuhusu utaratibu wa kufungua zabuni na hapa alisisitiza kwamba uwashirikishe wazabuni wenyewe, nisema hata sheria tuliyonayo sasa Sheria No.9 ya mwaka 2005, utaratibu huo upo ndani ya sheria na hata pale yanapotoka matangazo ya tenda, tangazo linaweka wazi kabisa tarehe ya ufunguzi wa tenda hiyo, tarehe ya ufunguzi wa zabuni hiyo inataja siku ile ile wakati tuna *Invalid Portent*. Lakini pia wanaarifiwa mahala na saa ambayo

tenda hiyo inafunguliwa na wale ambao wote wanahitaji kushiriki huwa hakuna kizuizi wanaruhusika kushiriki.

Kifungu cha 90, pia alikizungumza Mhe. Miraji, alizungumzia suala la aina za mikataba kwamba halikutolewa maelezo, ni kweli, kwenye Mswada huu ambao Waheshimiwa Wajumbe, mnao mikataba ile imetajwa tu lakini ilikuwa haijawekewa ufafanuzi, lakini Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wamepitia na wametoa ufafanuzi katika kila aina ya mkataba. Kwa hivyo, mkisoma marekebisho yao mtakuta kwamba mikataba hii imeainishwa kwa uwazi kabisa, lakini na pale ambapo patahitaji ufafanuzi zaidi basi tutauzingatia wakati tutakapotunga Kanuni za mswada wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nirudie kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yao na niombe sasa Mhe. Mwenyekiti, kuwasilisha rasmi majibu hayo naamini Waheshimiwa Wajumbe, wameridhika nayo na hawatasita kupitisha vifungu vya sheria hii, lakini pale ufafanuzi zaidi utakaohitajika basi tuko tayari kuutoa Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.
Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Hoja ilitolewa iamuliwe, wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa waliowafiki wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi pamoja na marekebisho yake, sehemu hii inaanzia kifungu cha 1 hadi kifungu cha 3.

Sehemu ya Pili

Mamlaka ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma pamoja na marekebisho yake, sehemu hii inaanzia kifungu cha 4 hadi kifungu cha 24.

Sehemu ya Tatu

Taasisi za Manunuzi na Uuzaji wa Mali pamoja na marekebisho yake kuanzia kifungu 25 hadi kifungu cha 44.

Sehemu ya Nne

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi niko kwenye kifungu cha 39(5) pamoja na marekebisho ya Kamati na maelezo aliyosema Mhe. Waziri, nilikuwa natatizo kidogo hapa naomba Mhe. Waziri, anipe ufafanuzi wa ziada, na naomba nisome marekebisho ambayo yatasomeka sasa katika kifungu cha 5, kinasomeka hivi;

"Wajumbe wanatakiwa wawe maafisa waandamizi wenye uzoefu kulindana na uzito wa kazi za ununuzi zinazotakiwa kufanywa".

Mara nyingi katika kukamilisha wajumbe hawa nazungumzia hasa katika taasisi za Serikali zile ambazo zina idara hazina Wakurugenzi wale unaowapata kwa kuchaguliwa na Rais, taratibu kwa kifungu hichi hivi kweli Mhe. Waziri, tutazisaidia taasisi zile za Serikali kwa maana ya Sheria hii ilivyokaa ya kifungu cha tano.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, suala la Mhe. Miraji, lililotaka ufafanuzi kwenye kifungu cha 39(5), kama kilivyorekebishwa na kamati, ni kwamba kifungu hichi kitatosheleza na kama nilivyotoa katika maelezo yangu wakati najibu hoja, ni kwamba maafisa waandamizi ni *senior officers* ambao watateuliwa na Afisa Mas-uul ambaye ndio mwenye jukumu na la kuwajibika moja kwa moja kwa shughuli zote za manunuzi, kwa hivyo, nina hakika kwamba Afisa Mas-uul au Afisa Mhasibu atachagua miongoni mwa watendaji wake waliochaguliwa na Mhe. Rais kushika idara, kama Katibu Mkuu watakaochaguliwa ni Wakuu wa Idara ambao wamechaguliwa na Mhe. Rais.

Lakini vile vile maafisa waandamizi wengine wawili ambao watatoka ndani ya Ofisi ile lakini vile vile watakaotoka katika Wizara inayohusika na fedha. Lakini hapa pia tumesema kuna mambo mengine ambayo yatafafanuliwa wakati wa utungaji wa Kanuni za sheria.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Idara ambazo nazizungumzia mimi za Serikali mara zote zinakuwa na mteuliwa mmoja tu kwa mfano Shirika la Bandari, lakini ziko idara nyingi za Serikali na maafisa waandamizi si

aghalabu mule kukutana nao, mara nyingi utakutana na wakuu wa Idara ambapo hapa Afisa Mas-uula tunategemea kuwa Mkurugenzi wa taasisi ile, uteuzi wake katika kipengele hiki na maafisa waandamizi hawa hasa taasisi zetu zilivyo inanipa mashaka sana na ndio maana nilikuwa nataka zaidi ufafanuzi wa Mhe. Waziri.

Lakini naomba tuendelee kwa sababu kanambia atakapokuja kutunga kanuni ile atazingatia zaidi eneo hili, nimuombe tu, taasisi nyingi za Serikali mara nyingi zina mteule mmoja, kunakuwa na idara ndogo ndogo ambazo zinakuwa zinamsaidia Afisa mas-uula, sasa si wakati tosha kukiweka kipengele hichi kama hatujakwenda kupeleka tafsiri nzuri ya kanuni zetu zitakazotusaidia kuweka sawa na kukipa uwezo mkubwa kitengo cha manunuzi katika Idara za Serikali. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Kwanza kwenye kifungu hichi alichokizungumza Mhe. Miraji, kinahusiana na kamati ya tathmini, sio ile *tender board,* lakini hata ile *tender board* kama nilivyosema tumeliona hilo alililoliona yeye kwamba zipo Idara za Serikali ambazo hazitokidhi vile viwango ambavyo tumeviweka, na hilo tulisema tutalizingatia kwenye kanuni kama alivyokwisha kusema, nilikuwa nataka kutoa ufafanuzi huo tu.

Sehemu ya Nne

Kanuni za Ununuzi na Uuzaji wa Mali amoja na marekebisho yake sehemu hii inaanza kifungu cha 45 hadi 48.

Sehemu ya Tano

Kanuni za Ununuzi na Uuzaji wa Mali pamoja na marekebisho yake sehemu hii inaanza kifungu cha 49 hadi 73.

Sehemu ya Sita

Utaratibu wa Ununuzi na Uuzaji wa Mali pamoja na marekebisho yake sehemu hii inaanzia kifungu cha 74 hadi 89.

Sehemu ya Saba

Aina za Mkataba pamoja na marekebisho yake sehemu hii inaanzia kifungu cha 90 hadi 91.

Sehemu ya Nane

Kuzingatiwa tena Mapitio na kukata rufaa pamoja na marekebisho yake sehemu hii inaanza kifungu cha 92 hadi 96.

Sehemu ya Tisa

Masharti mengineyo pamoja na marekebisho yake sehemu hii inaanzia kifungu cha 97 hadi 106.

(*Baraza lilirudia*)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya kutunga sheria imepitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu bila ya mabadiliko na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwa)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma 2016
(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya Mwaka 2016 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Muswada wa sheria ya serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nashukuru kwa mijadala yenu na michango yenu na hatimae kupitisha Mswada huu hapo ndio mwisho wa shughuli yetu. Naomba niahirishe Baraza hili hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 11.34 jioni Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 30/11/2016 saa 3.00 asubuhi)